Gazeti la kwanza la Kiislam kutolewa kwa lugha ya Kiswahili - mwaka 1936

Mapenzi ya Mungu

Mapenzi kwa wote bila chuki kwa yeyote

DAR ES SALAAM TANZANIA

JUZU 74 No. 181 | RAB. 2 - JUMD.2 1436 AH | FEB./MARCH 2015 | TAB./AMAN. 1394 HS | BEI TSH. 500/=

Nukuu ya Qur'an Tukufu

Enyi mlioamini! Mtiini Mwenyezi Mungu na Mtiini Mtume Wake na wale wenye mamlaka juu yenu; na kama mkigombana juu ya jambo lo lote, basi lirudisheni kwa Mwenyezi Mungu na Mtume, ikiwa mnamwamini Mwenyezi Mungu na siku ya Mwisho. Hiyo ndiyo heri, nayo ina matokeo bora. *(An-Nisaa 4:60).*

Khalifa mtukufu awaasa Waislamu:

Bila utii hakuna Amani

Na mwandishi wetu, Dar es Salaam

Katika hotuba yake ya Ijumaa ya tarehe 05/12/2014, Kiongozi mkuu wa Jumuiya ya Waislamu Waahamdiyya duniani, Hadhrat Mirza Masroor Ahmad, Khalifatul Masih V a.t.b.a., alizungumzia juu ya dhana nzima ya utii na umuhimu wake kwa ajili ya maendeleo ya Uislam na uanadamu kwa ujumla.

Baada ya kusoma tashahhud na suratul Faatiha Khalifa Mtukufu alisoma aya ifuatayo:

Enyi mlioamini! Mtiini Mwenyezi Mungu na Mtiini Mtume Wake na wale wenye mamlaka juu yenu; na kama mkigombana juu ya jambo lo lote, basi lirudisheni kwa Mwenyezi Mungu na Mtume, ikiwa mnamwamini Mwenyezi Mungu na siku ya Mwisho. Hiyo ndiyo heri, nayo ina matokeo bora. (4:60).

Kisha akasema:

Aya hii inaeleza kanuni ambayo waumini wa kweli wanatakiwa kuifuata. Kanuni yenyewe ni hii kwamba wasisitize juu ya haja ya kuwa watiifu na wajitahidi sana katika kufikia viwango vya juu vya utii, iwe ni utii kwa Mwenyezi Mungu, kwa mtume wake au kwa wale walio na mamlaka juu yao. Iwapo wale walio na mamlaka juu yao au serikali inawaelekeza kwenye jambo linalokwenda kinyume na amri iliyo wazi ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake , basi katika hali hiyo amri ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake ni lazima ipewe kipaumbele. Ingawaje iwapo kuna uhuru wa kuabudu / au serikali iliyopo inatoa uhuru wa kidini, basi hapo serikali au walio madarakani wawe ni waislamu au sio waislamu, ni lazima watiiwe.

Masihi Aliyeahidiwa a.s. amesema: Qurani tukufu inatumuru kwamba: Mtiini Mwenyezi Mungu na Mtiini Mtume Wake na wale wenye mamlaka juu yenu; …. Hapa inaamriwa kwa uwazi juu ya kuwatii wale walio na mamlaka na itakuwa ni jambo la kosa la wazi mtu kudhani kwamba serikali haziingii kwenye kauli hii ua "wenye mamlaka juu yenu" Chochote serikali inachosema katika mambo ya sheria kinaingia katika "wenye mamlaka juu yenu". Yeyote yule (mwenye mamlaka) asiyepingana nasi huyo yu pamoja nasi. Hivyo ni jambo lililothibitika kwa uwazi katika Kurani tukufu kwamba serikali ni lazima zitiiwe na chochote zitakachokisema kikubaliwe. ' (Journal Al Andaz, p. 69 – Tafseer Hazrat Masih e Maud,

Endelea uk. 2

Mtume Mtukufu Muhammad s.a.w:

Mfano uliokamilika kwa wanadamu

Imefasiriwa na Dawati la Kiswahili, Morogoro

(Ilitolewa na Hadhrat Mirza Bashiruddin Mahmood Ahmad, Khalifatul Masih II r.a. 26 Nov. 1933 wakati wa Jalsa ya Siratun Nabiyyi huko Qadian)

Baada ya kusoma Tashah hud, Ta'awwudh na Sura Fatiha Huzur r.a., alisema:

SHITAKA FULANI

Kabla ya kuyaanza madhumuni yenyewe, ninapenda kuongelea kuhusiana na andiko fulani ambalo nimepewa sasa hivi. Ndani yake mna saini za wahindu kadhaa na wamelalamika kwamba, leo maandamano fulani yamepitia mtaani kwao ambapo hakukuwa na desturi ya aina hii hapo kabla na tabia za baadhi ya wanafunzi walioshiriki humo hazikuwa zenye kupendeza.

Kabla ya mimi kufahamu kwamba ni tabia gani zisizopendeza walizozitenda, ambazo kuhusiana nazo kama watanifahamisha hapo baadae, basi hapo nitachukua hatua ya kila jambo lililokuwa halikupendeza. Lakini nasaha ya ujumla naitoa kabla ya kufanya uchunguzi, kwamba kama kuna yeyote yule aliyefanya jambo lisilopendeza, basi hilo lilikuwa ni jambo lisilopendeza kabisa.

Sisi tumeiteua siku hii kwa ajili ya jambo hili kwamba uweze kupatikana msingi wa suluhu na amani baina ya watu wa kaumu mbali mbali. Na siku ile ambayo tunataka kuifanya kuwa msingi wa suluhu baina ya watu wa kaumu mbali mbali na ambayo tunataka kuibadili taratibu katika sura hii kwamba watakatifu wa dini zote wakumbukwe kwa majina mazuri, ili ile chuki iliyomo baina ya watu wa dini mbali mbali iondoke na upendo uongezeke. Kuujeruhi moyo wa mtu katika siku hiyo, ambapo tangu mwanzo ni jambo lisilopendeza ndani ya mafundisho ya kiislamu na waislamu wameagizwa kujiepusha na jambo lile lenye kuwaudhi wengine, ni jambo lisilopendeza hasa. Na hasa katika siku hiyo inapaswa kulizingatia sana jambo hili kwamba lisifanyike jambo lolote lenye ku uudhi moyo wa mtu.

HASARA ZA MIPAKA BANDIA

Ninapenda kutoa rai yangu kuhusiana na Lalamiko lao hili kwamba hapo kabla hakukuwepo na desturi hii ya maandamano kupitia mtaani kwao, na rai yangu ni hii kwamba watu wa kaumu zote tunapaswa kuufutilia mbali ufinyu huu wa mawazo. Kwa rai yangu kadiri utakavyoendelea kuwepo mfarakano huu wa soko la wahindu, soko la waislamu na kitongoji cha wahindu na kitongoji cha waislamu, basi haitapatikana ndani mwetu hamasa ya kuongeza upendo kati yetu. Kutokana na mipaka hii ya bandia, mioyoni mtakuwemo na mafundo ya aina hii, ambayo yatatuzuia kukutana. Kile kitu chenye kujeruhi mioyo, kiwe kimefanyika katika kitongoji cha Wahindu au cha Waislamu, kwa vyovyote vile ni kibaya. Kama wahindu wawapo kitongojini kwao wawatukane waislamu au waislamu wawapo kitongojini kwao wawaseme vibaya Wahindu, basi hii bila shaka ni sahihi kwa sababu wengine hawakuyasikia matusi hayo ya wengine, kwa sababu hiyo jadhba haitaenea na fujo haitatokea. Lakini asili ya fujo hasa iko moyoni.

Kama muwepo katika maeneo yenu na kufunga milango, bali ndani ya vyumba vyenu au hata zaidi ya hapo, mtu fulani amnong'oneze mtu mwingine kwa kumtusi mtu fulani au hata kama amtusi kimoyomoyo, hata hivyo kitendo hicho kitakuwa bado ni kibaya, kwa sababu moyo wa yule atukanaye kimoyomoyo umeshaharibika na msingi wa upendo hauwezi kuwemo ndani ya moyo wa aina hiyo.

Ndio sababu kama urekebishaji wa mioyo uzingatiwe, basi hakuna mpaka wowote unaoruhusu kutukanana au kusemana vibaya, iwe kidhahiri au kisiri au katika vitongoji vyenu au katika vitongoji vya watu wengine. Lakini kama moyo haukuudhiwa na maandamano ya Wahindu yapitie kitongojini kwetu, sasa umo kuna uharibifu gani na kuna jambo gani humo la kulalamika. Au kama maandamano yetu yapitie kwenye kitongoji cha Wahindu bila ya kuleta maudhi yoyote sasa humo kutakuwa na dhara gani?

SABABU HASA YA VURUGU NCHINI INDIA

Lakini hiyo ni rai yangu binafsi, na hadi pale utakapokuwepo ndani ya kila mtu uvumilivu huu wa moyo, hadi wakati huo, kama

Endelea uk. 4

Mapenzi ya Mungu

Maoni ya Mhariri

SAFINA KWENYE GHARIKA

Mambo yanayoendelea katika ulimwengu wa Kiislam kwa hivi sasa hapana shaka yoyote ni matendo yasiyo na uhusiano hata kidogo na mafundisho aliyoyaweka mbele ya dunia mbora wa viumbe wote, bwana wa daraja, Mtukufu Mtume Muhammad (saw).

Kwa takribani miaka 23 Mtukufu Mtume Muhammad (saw) bila kuchoka au kupumzika aliendelea kufundisha, kueleza, kufafanua na kuweka bayana mafundisho ya Islam. Akayatoa kabisa mafundisho hayo katika kiwango cha nadharia na kuyaweka katika vitendo. Huu ulikuwa ni muujiza wa aina yake ambao hatuupati katika dini yoyote iwayo. Kiongozi wa dini kuonyesha kwa matendo katika mafundisho yote yaliyo katika kitabu chake kitakatifu. Historia ya Islam inatueleza ya kwamba mtukufu Mtume (saw) alivimba miguu katika ibada, aliandika barua kuwaita viongozi na watu kwa ujumla katika Islam, alitoa hotuba, ilmuradi maisha yake yote yalikuwa ni mahubiri jinsi gani Muislam anatakiwa kuishi.

Bahati tuliyonayo Waislam ni kwamba hakuna nyanja yoyote ile ambayo Mtume (saw) hakuionesha kwa matendo. Hivyo hatuna udhuru hata kidogo, tufanyeje na kwa wakati gani. Hayo yote yapo wazi kwetu. Tutatoa mifano michache. Alikuwa yatima na tukaoneshwa njia ya kuishi tukiwa yatima. Alikuwa mfanyabiashara akawaachia somo la uaminifu wa hali ya juu wafanya biashara wote, alikuwa kiongozi bila kujinaki na kunata na akaonesha kiongozi anatakiwa achukue njia ipi kuleta amani na maendeleo. Alilazimika kupigana na akaonesha kuwa si lazima kuacha utu wako wakati wa kitali (vita), alisamehe kusamehe kulipo faa, akaonesha huruma. Sisi Waislam tunakuwaje, tumesahau kwa haraka aliyotuonesha mpenzi kiongozi wetu Mtume Muhammad (saw), inasikitisha mno na kuumiza.

Maadui hivi leo wanatusimanga na kutuonesha vidole kwamba mafundisho yetu si lolote isipokuwa ubingwa wa kumwaga damu. Hii ni dhuluma kubwa sana, ukitambua ya kwamba maana ya neno Islam ni amani.

Lakini suala la kujiuliza ni je hivi watu wakipotea kiasi hicho, wakaenda mbali na nuru kiasi hicho, ni nguvu gani na mvuto gani unaoweza kuwarudisha kwenye nuru hiyo?

Ni dhahiri ya kwamba uwezo wa kuwarudisha kwenye nuru hiyo ili iangaze dunia ni kazi ya Muumbaji wa mbingu na ardhi. Kazi hiyo ameifanya kwa mafanikio makubwa Masihi Aliyeahidiwa Seyidna Ahmad (as).

Tutatoka katika giza hili, tutaondokana na mashaka haya, tukisikiliza sauti ya mpendwa wa Allah aliyeunda safina ya kutuvusha katika tufani hili ambalo limeigeuza dunia hii kuwa ni uwanja wa fujo.

Tunawaita wote wenye kuipenda Islam wafanye haraka kupanda safina aliyoiunda Masihi Aliyeahidiwa, ni katika safina hiyo tu ndipo tunapoweza kupata utulivu na shabaha hasa ya kuumbwa kwetu. Tusichelewe basi kwani 'ajizi ni nyumba ya njaa'.

Khalifa mtukufu awaasa Waislamu:

Kutoka uk. 1

Vol. II, p. 246))

Hivyo basi Yule ambaye ni Hakimu tena aliye mwadilifu wa zama hizi anasema kwa uwazi kwamba ukiondoa jambo ambalo kwa uwazi linapingana na amri ya Mungu na Mtume wake sheria ya nchi lazima itiiwe. Iwapo waislamu wataishika kanuni hii, vurugu na uvunjifu wa amani katika nchi nyingi za kiislamu zingetoweka kabisa.

Huzur alisoma nukuu ndefu kutoka maandishi ya Masihi Aliyeahidiwa a.s. ambamo alieleza mambo yafuatayo: Ni kipi kinatakiwa kiwe kwiango cha utiifu, maana ya utii, madhara ya kutokuwa na utii na nafasi ya utiifu katika kuieneza Islam. Katika zama zetu hizi ni Waahmadiyya tu wanaoweza kuonesha maana aya kweli ya utii na wanaweza kuionesha mfano dunia wa jinsi heshima ya Waislamu inavyoweza kuhuishwa / kusimamishwa.

Masihi Aliyeahidiwa a.s. ameandika: Yaani kwamba: Mtiini Mwenyezi Mungu na Mtume wake na watawala wenu. Iwapo utii utashikwa kwa ukweli na uaminifu, moyo hupata mwanga na roho hupata utulivu na nuru. Mazoezi ya kiroho hayahitajiki zaidi kuliko vile yanavyohitajika mazoezi ya utii, Ingawaje utii unatakiwa uwe wa uaminifu kabisa na hilo ndilo jambo gumu kweli kweli. Inakuwa ni lazima kuusagasaga ubinafsi wenu kwenye kinu cha utiifu kwa sababu haiwezekani kufikia utiifu wa kweli bila kufanya hivyo. Na ubinafsi ni hali ambayo inaweza kumfanya hata mtu anayeshikilia umoja wa Mungu ajitengenezee masanamu moyoni mwake. Baraka kubwa kiasi gani ilikuwa juu ya masahaba r.a. ambao walikuwa ni jumuiya iliyojitolea kwa moyo wote kumtii Mtukufu Mtume s.a.w.

Ni ukweli wa wazi kwamba jumuiya haiwezi kuwa jumuiya na haiwezi kuwa na ghera ya utaifa wao na mapatano hadi pale itakaposhikilia kanuni ya utii. Iwapo tofauti za kimawazo na mtengano zitapewa umuhimu zaidi basi elewa kwamba hiyo ni ishara ya bahati mbaya na kuangamia kwa jamii hiyo. Pamoja na sababu zingine nyingi, kutokukubaliana katika baadhi ya mambo na migongano ni miongoni mwa sababu za maanguko na hali dhofu ya waislamu. Iwapo tofauti za kimawazo zitawachwa na mtu mmoja tu atatiiwa, ambaye kutiiwa kwake kumeamriwa na Mwenyezi Mungu basi mafanikio yanapatikana katika kila kitu. Mkono wa Mwenyezi Mungu uko juu ya Jumuiya (yenye utii), na hapo ndipo ilipo siri ya mafanikio.

Mwenyezi Mungu amependelea kwamba Tauhidi yake na Umoja wake hauwezi kusimamishwa hadi pale utii utakapotekelezwa. Katika nyakati za Mtukufu Mtume s.a.w. maswahaba walikuwa ni watu wanaojiamini sana na walikuwa wenye maoni mazito ya kwao. Pia Mwenyezi Mungu aliwaumba wakiwa na vipawa vya kisiasa ndani yao. Jinsi Hadhrat Abubakar r.a. na Hahdrat Umar r.a. pamoja na masahaba wengine walivyouongoza utawala wakati walipopewa mamalaka inaonesha dhahiri walivyokuwa na vipaji hivyo kwa kiwango cha hali ya juu kabisa. Ingawaje wakati Mtukufu Mtume s.a.w. alipokuwa pamoja nao hawakuyahesabu mawazo yao na vipaji vyao kuwa chochote. Chochote alichokisema Mtukufu Mtume s.a.w. wakichukua kuwa ni cha lazima na cha mwanzo kutetekelezwa. Walijitoa kwa kumtii kiasi hiki kwamba walihesabu hata maji yaliyodondoka wakati akiweka udhu kuwa ni yenye baraka na maji yake aliyosukutua mdomo kuwa ni matakatifu. Kama hawangelikuwa na kiwango hiki cha utiifu na kumkubali na kama kila mmoja wao angelitoa umuhimu kwa wazo lake na kuliona kuwa bora basi lazima kungelikuwa na migongano kati yao na kamwe wasingelifikia daraja za juu walizozifikia.

Kwa maoni yangu hoja moja tu inatosha kuandoa tofauti iliyopo baina ya sunni na Shia na hoja hiyo ni kwamba masahaba wa Mtukufu Mtume s.a.w. r.a. hawakuwa na mtengano na uadui kati yao. Maendeleo yao na ufaulu wao ni dalili inayothibitisha kwamba walikuwa kama kitu kimoja na hakukuwa na hata mmoja aliyekuwa na uadui na mwenzake. Wapinzani wajinga wa Islam wanatangaza kwamba Islam ilienezwa kwa nguvu ya kulazimisha lakini ninasema kwamba hiyo sio sahihi. Uhakika ni huu kwamba (nyoyo za masahaba) ziligubikwa na roho ya utii na ni matokeo ya utii na umoja wao ndipo wakaweza kuzishinda nyoyo. Imani yangu ni hii kwamba walichomoa panga zao pale tu walipolazimika kujilinda. Na hata kama wasingechomowa panga zao kwa hakika wangeishinda dunia kutoka na kauli zao.

Hakuna shaka kwamba maneno yanayotoka moyoni huuathiri moyo mwingine.

Masahaba r.a. waliukubali ukweli kwa uaminifu wote na hakukuwa na kujisingizia kokote. Ukweli wao wenyewe ukawa chanzo cha ufaulu wao. Ni jambo sahihi kwamba mtu

Endelea uk. 3

Namkumbuka Bi Radhia

Mhariri Mapenzi ya Mungu Assalaam Alaikum warahmatullah wabarakaatuh. Tafadhali sana naomba uchapishe Makala haya katika gazeti lako na kisha unitumie nakala ya gazeti ulimotoa makala haya.

Radhia Amri Abedi Kaluta

Radhia alikuwa binti wa Sheikh Kaluta Amri Abedi. Alishiriki katika shughuli za Jamaat kwa huba na jazba kubwa. Elimu yake kuhusu mafundisho ya Jamaat na Islam kwa jumla ilikuwa nzuri. Shauku yake ya kuhubiri Ahmadiyya haikuwa na kikomo. Alikuwa na roho nzuri na mkarimu. Na kwa hakika alikuwa na mkono wa kutoa. Na kila nilipotembelea Tanzania hakukosa kuja kunitazama na kutengeneza kashata kwa ajili ya familia yangu.

Radhia alidumu katika kusimamisha ibada Msikitini. Alikuwa na utii wa hali ya juu kwa nidhamu ya Ukhalifa. Kwa muda alikuwa Rais wa Lajna (Tanzimu ya akina mama wa Kiahmadiyya). Akiwa Rais wa Lajna alitoa mchango mkubwa kwa Tanzimu hiyo. Mapenzi yake ya kuitumikia Jamaat daima yalinikumbusha baba yake.

Uwezo wake katika lugha ya Kiingereza na Kiswahili ulikuwa ni mzuri na alikuwa ni miongoni mwa wataalamu wa kuchunguza tafsiri ya vitabu vya Jamaat. Na alibahatika kutimiza nguzo ya Hija. Mwenyezi Mungu Amlaze kwa amani na salama. Amin

Mohammed Iqbar Dar
Birmingham – U.K

BODI YA UHARIRI

Msimamizi: Sheikh Tahir M. Chaudhry - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri: Mahmood Hamsin Mubiru.
Kompyuta: Abdurahman M. Ame.
Mchapishaji: Sheikh Muhammad Arif
Msambazaji: Mwl. Omar Mnungu
Wajumbe: 1. Abdullah Khamis Mbanga
2. Swaleh Kitabu Pazi
3. Jamil Mwanga.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed S.L.P. 376.
Simu 022 - 2110473, Fax 022 - 2121744, Dar es Salaam, Tanzania.
Email: mapenziyamungu@yahoo.com

Khalifa mtukufu awaasa Waislamu:

Kutoka uk. 2

mkweli siku zote hutumia nguvu za ukweli wake. Dhati iliyobarikiwa ya Mtukufu Mtume s.a.w. ilizalisha mwanga wa kumtegemea Mungu kwa uzuri na utukufu. Ilikuwa na mvuto na nguvu ya kuzivuta nyoyo. Na Jumuiya yake ikawa ni mfano wa kuigwa kwa utii wao kwa Mtukufu Mtume s.a.w. na uimara wao ulithibitika kuwa wa juu kabisa kiasi hiki kwamba yeyote aliyoeuona hakuwa na njia isipokuwa kuvutwa nao. Kwa ufupi kuna haja kubwa leo kuihuisha hali ya umoja waliokuwa nao masahaba r.a. Kwa sababu Mwenyezi Mungu ameiunganisha Jumuiya ambayo inapewa mafunzo kwa mkono wa Masihi Aliyeahidiwa a.s. kuwa sawa na Jumuiya iliyopata mafunzo ya Mtukufu Mtume s.a.w., mafanikio ya Jumuiya yatapatikana tu pale tutakapoiga mfano wa watu hao (masahab) pekee. Hivyo basi ninyi nyote mnaojihesabu kuwa wa Jumuiya ya Masihi Aliyeahidiwa a.s. na iwapo mnapenda muunganishwe na Jumuiya ya masahaba basi zalisheni ndani yenu hali hiyo ya masahaba. Igeni utii wao, igeni mapenzi yao na umoja uliokuwa baina yao. Kwa ufupi shikeni njia za masahaba katika kila hali. (Al Hakm, Vol. 5, dated 10 February 1901, pp. 1-6)

Masihi Aliyeahidiwa a.s. amefafanua aina mbalimbali za utii kwenye nukuu hii. Kwanza ameelezea utii kwa Mwenyezi Mungu, kisha utii kwa Mtume wake kisha utii kwa wenye mamlaka / watawala na utii kwa serkali pia. Utii kwa wenye mamlaka unaingiza utii kwa serikali na utii kwa uongozi wa jamaat. Utii kwa Ukhalifa unatakiwa uwe juu kuliko utii kwa serikali na utii kwa uongozi wa Jamaat kwa sababu Khalifa anasimamia moja kwa moja amri za Mwenyezi Mungu na Mtume wake na uongozi wa Jumuiya unafanya kazi chini ya Khalifa. Ni katika uzuri wa Ukhalifa kwamba wakati wowote kunapotokea kutofautiana baina ya wale walioteuliwa kushika nyadhifa mbalimbali za kiuongozi na wanajumuiya wa kawaida, basi khalifa wa zama hukimbilia kuondoa tofauti hizo. Kwa hakika hilo ni moja kati ya majukumu / kazi za khalifa na daima hufanya hivyo. Hivyo utii kwa Ukhalifa unakuja kabla ya utii kwa serikali. Ingawaje hakutakiwi kuwa na uelewa usio sahihi katika hili kwa sababu Khalifa wa zama mwenyewe siku zote anakuwa wa mwanzo katika kutii sheria za nchi na huwahimiza wengine kufanya hivyo.

Masihi Aliyeahidiwa a.s. amesema mahala pengine kwamba kwa msemo wa kidunia 'ulul amr' (yaani wenye mamlaka) inamanisha wafalme na katika msemo wa kiroho inamanisha Imam wa zama (The Need for The Imam, p. 37).

Kwenye mipaka hiyo hiyo ya uongozi wa serikali za kidunia mfumo wa utawala wa kiroho unaweza pia kufanya kazi. Bahati njema ni yetu basi kwa kuwa sehemu ya mfumo huo wa utawala wa kiroho. Ukhalifa daima hujitahidi kusimamisha Ufalme wa Mungu na Mtume wake ndani ya nyoyo na akili za watu na wakati wowote kunapotokea kutofautiana Khalifa hutoa maamuzi sawa na amri za Mungu na Mtume wake. Ni hisani ya Mwenyezi Mungu kwamba tunao utaratibu wa ukhalifa kati yetu, vinginevyo makundi mbalimbali ya waislamu yanazo tofauti za kifikihi kwenye mambo mbalimbali zinazowagawa, na badala ya kujaribu kuziondoa tofauti zao kila siku wanazidi kuachana. Hivyo hivyo maswala mabalimbali yanaweza kusabisha mtengano ndani ya serkali pia. Basi tofauti ya kimawazo kwenye maswala mbalimbali (na watu wakabaki kuwa wamoja) inaweza kupatikana tu chini ya Ukhalifa. Waahmadiyya hawawezi kutoa shukurani ya kweli kwa hisani hii hadi pale watakapoonyesha utii wa moja kwa moja na uliokamilika kwa Ukhalifa.

Masihi Aliyeahidiwa a.s. alisema kitu kimoja muhimu sana: Iwapo utii utashikwa kwa uaminifu kabisa basi nyoyo hupata mwanga na roho hupata utulivu na nuru. Kwa hakika hapa utii unaokusudiwa ni ule wa mfumo wa kiroho na hiki ni kipimo cha kupimia kiwango cha utii wa kila mtu katika ngazi binafsi. Je unaupata utulivu na nuru iliyotajwa hapa. Tafakari wewe mwenyewe juu ya kiwango chako cha utii na kisha jipime wewe mwenyewe ni kiasi gani cha utii ulichonacho juu ya Mwenyezi Mungu, juu ya Mtume wake na juu ya Ukhalifa ulioanzishwa na Masihi Aliyeahidiwa a.s. Utii wa mamlaka za kiserikali hupelekea amani na utulifu lakini utii kwa mamlaka ya utawala wa kiroho hupelekea amani ya moyo na faraja. Masihi Aliyeahidiwa a.s. amesema: Mazoezi ya kiroho hayahitajiki zaidi kuliko unavyohitajika utii ... kwani bila ya huo mtu hawezi kamwe kuuona mwanga wa kiroho na utulivu wa moyo kwenye maisha yake yote. Watu wanajioamini kwenye kutekeleza sala zao na kumuabudu kwao Mungu lakini hawatekelezi utii wowote hawawezi kupokea baraka / fadhili za Mwenyezi Mungu.

Aina nyingine ya kufikia viwango bora vya utii iliyoelezwa na Masihi Aliyeahidiwa a.s. ni hii kwamba: Ni jambo la lazima kuusagasaga ubinafsi wenu kwenye kinu cha utii .. mtu ajilazimishe kuyafanya matakwa yake yaendane na amri ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake ili aweze kufikia utii wa kweli. Masihi Aliyeahidiwa a.s. amesema masanamu yanaweza kuzalika hata ndani ya nyoyo za wale wanaoshikilia umoja wa Mungu na wasiweze kuwa watii hata katika mambo madogo madogo tu. Masihi Aliyeahidiwa a.s. amesema pia masahaba wa Mtukufu Mtume s.a.w. waliweza kufikia viwango vya juu vya uchamungu kwa sababu tu walijitahidi kutekeleza utii.

Kwa hakika hadithi zinaeleza kwamba hata kama mtumwa mweusi anawekwa kuwa kiongozi wenu ni lazima mumtii. Katika mapokezi mengine imesemwa hata kama kichwa cha kiongozi wenu kiko kama zabibu iliyooza basi ni lazima mumtii.

Masihi Aliyeahidiwa a.s. amelinganisha maendeleo ya jamii / jumuiya na utii na amesema kwamba jamii / jumuiya haiweza kuwa jamii kweli au jumuiya kweli hadi pale watu wake watakaposhikilia utii na hapo ndipo ilipo siri ya maendeleo. Mtukufu Mtume s.a.w. alisema: Maendeleo yapo katika kushikamana na Jumuiya, katika kumsikiliza kiongozi wa zama na katika kumtii. Iwapo uma tu wa Kiislamu duniani ungeweza kuelewa jambo hili ungekuwa ni nguvu kubwa sana ambayo hakungekuwa na nguvu yoyote nyingine ambayo ingeweza kupambana nayo. Sisi Waahamdiyya basi, ni lazima tufikie viwango vya juu vya utii. Mwenyezi Mungu amesema kwamba kwa ajili ya jumuiya za kiroho utii ni sharti muhimu na la lazima katika kupata matunda mazuri / kupata mafanikio. Ingawaje pia utii unaleta matokeo yenye kushangaza hata kwenye jumuiya za kidunia.

Hazrat Musleh Maud r.a. alitaja mfano huu wa Napoleon kurudi kwenye madaraka yake na akasema 'Napoleon na viongozi wengine wa kidunia kama yeye hawakuwa na ahadi ya msaada wa Mungu pamoja nao, msaada ambao waumini wa kweli wameahidiwa, lakini pamoja na hayo bado waliweza kuleta mapinduzi makubwa sana. Bila shaka hali ya wale waliochukua baiat ni tofauti kabisa. Kwa hakika maana hasa ya bait ni kujiuza na kujiingiza katika utiifu moja kwa moja. Maana hii ya baiat ni ya ndani kabisa na iko juu kiasi hiki kwamba utii wa kidunia hauwezi kulinga nayo hata kwa mbali. Agizo hili: Mtiini Mtume Wake na wale wenye mamlaka juu yenu; ni la muhimu kiasi hiki kwamba iwapo taifa lolote halitolifuata, ama wawe ni warithi wa imani ya kweli au hawana habari nayo, taifa hilo haliwezi kufanikiwa.

Siku zote tuyaweke maneno ya Masihi Aliyeahidiwa a.s. mbele ya macho yetu kwamba ni muhimu tuwe na maelewano na utii ili tuwe kweli Jumuiya. Bila ya hayo tutaona maanguko na uozo. Quran tukufu inasema juu ya hili:

Na shikeni kamba ya Mwenyezi Mungu nyote, wala msiachane; na kumbukeni neema ya Mwenyezi Mungu iliyo juu yenu mlipokuwa maadui naye Akaziunganisha nyoyo zenu, hivyo kwa neema yake mkawa ndugu; na mlikuwa ukingoni mwa shimo la moto naye Akawaokoeni nalo. Hivyo ndivyo Mwenyezi Mungu Anavyokubainishieni Aya Zake ili mpate kuongoka. (3:104)

Ni jambo la bahati mbaya kwamba pamoja na agizo hili la wazi la kiungu waislamu wameanguka chini kabisa katika jambo la mapatano na wamesahau neema zilizo juu yao na wapo kwenye kipindi kigumu sana cha maanguko na maangamizi. Bila shaka muanguko huu umekuwepo tangu zama za Masihi Aliyeahidiwa a.s. lakini leo umefikia daraja yake ya chini kabisa. Masihi Aliyeahidiwa a.s. amesema: wacheni tofauti zenu na mtii yule mtu mmoja, yaani Imam wa zama, kisha muone jinsi kila kitu kitakavyobadilika kuwa neema kwa ajili yenu. Mwenyezi Mungu awape uoni wa hili.

Masihi Aliyeahidiwa a.s. amesema; Mkono wa Mwenyezi Mungu aliyetukuka uko juu ya Jumuiya .. na bila ya huo mafanaikio hayawezi kufikia na Mungu hawezi kuonekana. Mungu huonekana tu wale na haki wale tu na walio na uelewa wa kweli wa Umoja wa Mungu na pia wanao umoja miongoni mwao. Hatutakiwi kamwe turidhike tu kwamba tumefanya Baiat, bali tunahitajika tufikie viwango vya kufanya baiat ambapo kama inavyoeleweka kutoka kwenye maana ya baiat ni mtu kujiuza dhati yake.

Masihi Aliyeahidiwa a.s. alitoa mfano kwamba jinsi Hadhrat Abubakar r.a. na Hahdrat Umar r.a. pamoja na masahaba wengine walivyouongoza utawala wakati walipopewa mamlaka inaonesha dhahiri walivyokuwa na vipaji hivyo kwa kiwango cha hali ya juu kabisa. Ingawaje wakati Mtukufu Mtume s.a.w. alipokuwa pamoja nao hawakuyahesabu mawazo yao na vipaji vyao kuwa chochote. Chochote alichokisema Mtukufu Mtume s.a.w. walikichukua kuwa ni cha lazima na cha mwanzo kutetekelezwa.

Lakini pamoja na ukimya wao baadae dunia ilishuhudia jinsi walivyoongoza walipokuwa Khulafaa Rashideen.

Tukiongelea kwa ujumla, kwa fadhili za Allah Jumuiya inao moyo mkubwa wa utii ingawaje baadhi ya nyakati watu wasio wazuri wanapoondolewa kwenye nafasi za kiofisi, wanaanza kuuliza ni kwa nini wameondolewa, wao wana kasoro gani n.k. Iwapo mifano tuliyonayo kwenye historia itaweza kuzingatiwa hakuna nafasi ya kuzuka kwa maswali kama hayo.

Ni lazima tuzingatie kwamba leo ni Qurani ile ile na ni Mtume Yule Yule s.a.w. ambaye anafuatwa (au anadaiwa kufuatwa), lakini angali hali za waislamu. Ama wamegubikwa na migogoro au wanaipigia magoti dunia kuiomba. Masihi Aliyeahidiwa a.s. amesema tofauti za Shia na sunni zinatokana tu na kuachana kwao na utii. Kinachohitajika bila shaka ni umoja na hasa Masihi Aliyeahidiwa a.s. ameiomba Jumuiya yake ijitahidi kuwa na umoja kati yao kwa kiwango cha mfano wa masahaba ili kwamba ukweli wenu uukate uadui vipande vipande. Na hili litaweza tu kutokea pale ambapo kila mmoja wetu atajaribu na kujitahidi kuwa mtiifu na mnyenyekevu. Tutakapokuwa na utii kamili kwa Mungu na Mtume Wake ni hapo nasi tutakapoweza kupata sehemu ya mwanga ule aliopewa Mtukufu Mtume s.a.w..

Jukumu la Waahamdiyya ni kubwa sana, ni lazima tuoneshe kwa matendo mfano wa Mtiini Mtume Wake na wale wenye mamlaka juu yenu;.... jambo ambalo litaivuta dunia kujia kwetu. Hii ndio njia pekee tunayoweza kuifikisha dunia chini ya miguu au kizingiti cha Mwenyezi Mungu na Mtume wake na kisha tukaweza kuiongoza. Hii ndio njia pekee tunayoweza kuondoa mizozo na migogoro duniani. Tunazo amri za Kurani ambazo zinayo ahadi na thamani ya kuweza kufuatwa na kutiiwa. Tunao mfano uliobarikiwa wa Mtukufu Mtume s.a.w. na tunao wajibu wa kuufuata. Na pia tunao mfumo wa kiroho wa 'ulul amr' (wale wenye mamlaka) kati yetu / juu yetu ambao daima unaendelea kutukumbusha juu ya kutii amri za Mwenyezi Mungu na Mtume wake.

Basi hakuna sababu tena kwamba kusiwepo na tofauti ya wazi kabisa kati yetu na wengine.

Mwenyezi Mungu atuwezesha sote kutekeleza hayo na atuwezeshe daima kukwea vilele ambavyo vilivyokuwa ndio matarajio na matazamio ya Masihi Aliyeahidiwa a.s. kwa wafuasi wake. Amin.

Mtume Mtukufu Muhammad s.a.w. ni mfano uliokamilika

Kutoka uk. 1

yeyote aendelee kulalamika, basi inapaswa kitongoji hicho kiachwe (kufanyiwa maandamano). Lakini rai yangu ni hii hii kwamba inapaswa kuiondoa hali hii ya kutokuwa na uvumilivu kwa ajili ya kustawisha suluhu na amani. Na yale mambo ambayo hayakuelezwa na dini zetu, kwa mfano kitongoji cha wahindu, kitongoji cha waislamu, hakuna dini yoyote iliyoyaeleza, basi kwa nini tujiwekee tu mipaka mipya bila sababu yoyote. Magomvi yote hapa India huzalika kutokana na ufinyu wa aina hii hii wa mawazo ambayo daima mimi hupingana nayo.

UPEVU WA MOYO WA WAAHMADIYYA

Chini ya msikiti wetu mdogo hupita maandamano ya sherehe za wahindu, waislamu na masingasinga wakipiga ngoma na huwa wakipita hata katika wakati wa sala nikiwa nasalisha, lakini mimi sijawahi hata mara moja kuwazuia, bali baadhi ya watu walitaka kuwazuia lakini mimi nikawakataza. Kama mtu yeyote atutoe kwenye mawazo yetu kutokana na upigaji wake wa tarumbeta, sasa tutakuwa tumeyaelekeza vipi mawazo yetu kwenye dini. Yapaswa kwamba tujizamishe ndani ya dini kwa kiasi hiki kwamba kusiwe na kitu chochote kitakachoweza kututoa kimawazo tukielekee. Mimi sijawahi wakati wowote kukihisi hicho bali kama kuna yeyote aliyekihisi, basi mimi nilimkataza na kumwambia haya haya kwamba huu ni mtaa wa kupitiwa na watu na hadi sasa maandamano ya wote, wahindu masingasinga, waislamu, hupita hapo. Maandamano ya hapa na hata ya nje pia na ni rai yangu kwamba hii ndio njia ya kupatia suluhu.

Mambo yasiyopendeza, kwa hali yoyote ile, yawe ndani ya vitongoji vya wahindu au ndani ya vitongoji vyetu wenyewe, yanabaki tu kuwa ni yasiyopendeza. Kutokana na mawazo ya fujo, kama mtu aende kwenye kitongoji cha wengine na ifanyike harakati mbaya, basi hili linakuwa ni jambo baya zaidi. Lakini jambo lile lisilokuwa la kupendeza, basi hilo lisifanywe hata katika kitongoji chako mwenyewe.

NASAHA KWA JUMUIYA

Ndio sababu mimi napenda kusema bila ya kufanya uchunguzi wowote kwamba kama kuna yeyote aliyefanya harakati ya aina hiyo, basi atubu na kama hakufanya basi awe mwangalifu zaidi kwa siku za usoni. Na kama kuna kaumu yoyote haipendi upite mtaani kwake basi usipite. Lakini hata hivyo nitasema tena kwamba hiyo si njia ya suluhu. Kutokana nayo fujo inaendelea kutokea kila mahali na kwa kila watu. Na ni kutokana na mambo ya aina hii hii fujo huendelea kutokea baina ya wahindu na waislamu na katika maeneo ya Madras kati ya wahindu na wakristo. Wazo hili kwamba ni fedheha kwa mtu yeyote kupita kwenye maeneo ya msikiti au kitongoji si sawa hata kidogo. Kama yeye ni ndugu yetu sasa kuna kuwaje na fedheha katika jambo hilo. Lakini maadamu moyo haubadiliki na mwingine anaudhika, basi hadi wakati huo kama sisi tuache kuna dhara gani?

UPANA WA MADHUMUNI NA UFINYU WA WAKATI

Baada ya hayo ninapenda kusema kuhusiana na kusudio ambalo lililosababisha kundwa kwa Jalsa hii. Humo matukio ya kina ya Mtume s.a.w.hayawezi asilan kubainishwa kwa sababu wakati ni mdogo mno, ni siku za baridi. Kwanza kati ya sala za Adhuhuri na Alasiri kulikuwa na mapumziko ya saa moja na nusu hivi, humo wakati mwingine ulikuwa ukitumika katika kuwasili hapa na wakati mwingine katika kusoma Kurani na Mashairi. Kisha ulikuwa ukitumika katika kusimama na katika maneno ya awali na zilikuwa zikisalia dakika kumi na tano tu au ishirini. Na ni nani yule ambaye katika muda huu mfupi tu awezaye kuivuka bahari hii isiyo na kingo? Yawezekana tu kwa kiasi hiki kwamba baadhi ya amali za Mtume s.a.w. zielezwe ili elimu na upendo viongezeke kwa waliomuamini na chuki ipungue kwa wengine.

MAKUSUDIO HASA YA DINI

Leo nitaelezea kuhusiana na jambo hili kwamba dini zote zilizopo duniani zinakiri kwamba makusudio yao ni kumpata Mwenyezi Mungu. wahindu, Waislamu, Masingasinga, Wakristo, Wazartashti, Wayahudi, Wamajusi, kila mmoja anasema kuwa makusudio hasa ya dini yake ni kumpata Mwenyezi Mungu. lakini wote wanadai kuwa kumpata huko kutakuwa ni baada ya kufa. Kwa mfano itikadi ya Wasanatan Dharam ni hii kwamba baada ya kufa, watu waliokamilika hupenya ndani ya Mwenyezi Mungu. Waarya wanasema kwamba wao huenda kwenye ukaribu na Mwenyezi Mungu kwa muda mrefu. Hata wabudha nao wana itikadi ya aina hii hii. Wako baadhi ya Wayahudi ambao hawaiamini Kiama, wenye kuiamini hufahamu hivi hivi. Wazartashti, Waislamu, kwa uchache wote ni wenye wazo hili hili na wote wameiweka zama za kukutana na Mungu kuwa ni baada ya mauti.

Lakini sisi twaona kwamba hata mtu aliye safarini hujifanyia maandalizi fulani. Kwa hiyo hata duniani pia ambayo ni namna ya safari, kunapaswa kuwepo na mapendekezo ya kukutana na Mwenyezi Mungu na kuhusiana na hili, dini zote zimekubaliana kwamba mtu aendelee kuziiga sifa Zake (Mungu) hadi aupatapo ukaribu wa kweli na Mwenyezi Mungu, basi huo pia unakuwa ni ukaribu wa aina fulani. Kwa mfano saumu ni nini? Ni hii kwamba mwanadamu, kama Alivyo Mwenyezi Mungu, ajizuie kula kwa wakati fulani. Kisha sala ambayo mradi wake ni huu kwamba kama vile Mwenyezi Mungu, bila ya kuwa na mshirika yeyote, mwenzi au jamaa, vivyo hivyo mwanadamu pia, kwa wakati fulani, atengane na wenzake na jamaa zake. Na kwa namna hii ndani ya kila dini kuna ibada za aina fulani fulani na dini zote zimeafikiana katika jambo hili kwamba makusudio hasa ya maisha ya mwanadamu ni kuupata ukaribu na Mwenyezi Mungu na mfano wake duniani ni kujenga sifa za Mwenyezi Mungu ndani ya moyo. Na mtu aliyekamilika atakuwa ni yule yule atakayedhihirisha ndani ya dhati yake sifa zaidi za Mwenyezi Mungu.

MDHIHIRISHO KAMILI WA SIFA ZA MWENYEZI MUNGU

Ndani ya mada ya leo, nitaichukua na kuieleza, miongoni mwa kazi zake, kazi ile inayodhihirisha kuwa ni kwa kiasi gani aliziiga sifa za Mwenyezi Mungu na ambao mfano wake haupatikani kwingine kokote kule na ni kwa kusudio hili hili nilisoma sura ya Al Fatiha mwanzoni.

SIFA ZA UMOLA (RUBUUBIYYAT)

Ndani ya sura hii zimeelezwa sifa nne za Mwenyezi Mungu, ya kwanza ni Rabbul 'aalamiin. Popote utazamapo Umola wa Mwenyezi Mungu unafanya kazi, ardhi, mbingu, jua, mwezi, nyota, mashariki, magharibi, weupe, weusi, waasia, wazungu, wote wako chini ya Umola Wake nao wawe wadogo, wakubwa, matajiri, masikini, wote Anawalea.

SIFA ZA UWINGI WA REHEMA

Sifa ya pili ni Rahman (Mwingi wa Rehema), yaani nguvu zote zilizomo ndani ya mwanadamu Yeye Hutoa pia sababu za matumizi yake. Jambo hili halipo ndani ya serikali za kidunia. Kwa mfano vyuo vikuu husaidia kutoa elimu, lakini sio kwamba ni lazima baadae vimtafutie mtu ajira. Husema kwamba sisi tumefundisha sasa nenda katafute kazi. Hutoa tu elimu lakini haitoi njia za kuitumia. Lakini Allah ni Rahman, yaani Hutoa pia njia za kuutumia uwezo huo.

MAELEZO LATWIFU YA RAHMAANIYYAT

Kila kitu Alichokiumba, mkabala nacho Ametengeneza pia njia ya kuitumia. Kwa mfano jicho lahitaji mwanga ili liweze kuona, kwa hiyo Akaumba jua. Kisha ni muhimu kwamba jicho lione vitu vizuri ili mburudiko upatikane ndani mwake na hivyo Akaumba vitu kama vile mandhari nzuri, mbogamboga, mtu mzuri, wanyama, ndege, miti, mimea n.k.

Kisha Akaumba sikio, lakini Hakusema hivi kwamba wenyewe mjitengenezee sauti, bali Akaiumba pia na sauti. Kisha kuna tofauti zisizo na hesabu katika usikiaji wa sauti. Kama sauti za wote zingekuwa za aina moja, basi ingekuwa vigumu kuzitambua. Lakini mna tofauti ndogo kiasi ya kwamba mtu hustaajabu. Gari inakuja, farasi anakuja, lakini sikio linazitambua sauti zote hizo mbili.

Halafu kuna tofauti fulani fulani katika sauti za kila mtu. Hivyo kuna tofauti nyingi kiasi ya kwamba zikitazamwa hizo tu basi huonekana malaki ya kazi za sikio. Kisha Ameumba uwezo wa kugusa, lakini Hakusema hivi kwamba jitafutie mwenyewe kazi yake, bali Aliumba pia vitu kwa ajili kuvigusa. Kuna kitu laini, kingine kigumu, kingine chenye kuteleza na kingine chenye kukwaruza. Pia humo katika kila kimoja kuna aina nyingi. Kuna maelfu ya tofauti ndani ya ulaini. Huwa tunashika hariri na pia huwa tunashika mpira. Vyote ni laini, lakini uwezo wetu wa kugusa unavitofautisha vyote viwili na kwa namna hii kuna maelfu ya utofautishaji ndani ya ulaini. Hivyo sifa ya Rahmaniyyat ya Mwenyezi Mungu ilizozitoa nguvu kwa mwanadamu, Aliumba pia njia za kuzitumia. Lakini serikali za kidunia huwa hazifanyi namna hiyo.

MFANO WENYE KUPENDEZA

Mfano wake ni wa aina hii kwamba inasemwa kwamba mtu fulani alikwenda kuwinda na akamuua sungura na kumleta. Alipokaribia nyumbani likamjia wazo kwamba familia yangu ni kubwa, kuna watoto wadogo, dada zangu na ndugu zangu. Kama nitampeleka huyu sungura nyumbani basi watagombana. Hivyo ni bora nimpe mtu yeyote wa nje. Alikuweko Daruweshi akipita karibu yake. Basi akawaza kwamba acha nimpatie huyu huyu na katika mawazo haya akamuuliza, Ewe bwana! Unakula sungura? Lakini kabla hajamjibu likamjia wazo kwamba watoto watagombea minofu baada ya nyama kuiva. Lakini kama nimtoe nje, basi nitakapofika tu nyumbani wote wataniuliza je umetuletea nini? Kisha nitawajibu nini. Hivyo ni bora niipeleke nyumbani. Yule Daruweshi naye akamjibu swali lake kwa kusema: Naam nikipata nitakula tu. Kisha akasema; Vizuri! Basi uwinde ili upate kuwa unakula. Hivyo mifano ya serikali za kidunia ni hivi hivi kwamba baada ya kutumainisha kote huko husema windeni wenyewe ili mpate kula. Ndio sababu vijana walioelimika, ambao kuhusiana nao mtu fulani alisema kwamba kwa nini mmenidhalilisha baada ya kunipatia shahada ya uzamili. Wanasema vizuri, basi sisi tutawaueni kwanza. Na hao hao watu wenye elimu, ambao serikali baada ya kuwasomesha, haikuwaandalia mazingira ya kufanya kazi, basi huanza kuwaua watu wa serikali.

SIFA ZA RABBUL 'AALAMIIN NA MTUME S.A.W.

Hivyo nilikuwa nikieleza kwamba sifa ya kwanza ya Mwenyezi Mungu iliyoelezwa katika sura hii ni ya Rabbul 'Aalamiin. Yule mja anayekuwa Rabbul 'Aalamiin basi sisi tutafahamu kwamba huyo amekamilika, nasi tunaona kuhusiana na Mtume s.a.w. kwamba, je yeye alikitazama kila kitu ulimwenguni na kufanya kazi kwa ajili ya kukinufaisha? Kama alifanya, basi ni lazima itaaminika kwamba yeye alikuwa ni mwanadamu mkamilifu.

Lakini kama mtazamo wake haukukiangukia kila kitu na kukawa na sehemu zilizobakia ambazo hakuzifanyia kazi yoyote, basi hapo hawezi kusemwa kuwa ni Mola wa walimwengu. Kwa ajili yake twauchukua mfano wowote ule na kwa kuwa ni vizazi vya wanadamu vinavyojadiliwa, ndio sababu tunaleta mfano wa Adam ambaye kila kaumu inamkubali na ambaye Mwenyezi Mungu Alimfanya kuwa mbegu ya vizazi vijavyo. Yapaswa kutafakari kwamba tashi lake la kwanza litakuwa ni lipi? Yathibitika pia ndani ya Biblia, kwamba akili nayo yasema hivi hivi, kuwa kiwezacho kumpa utulivu ni lazima kiwe mwenzi wa jinsi yake. Uzuri wa dunia na kitu chake chochote kile, hakiwezi kumpa utulivu, maadam hayupo mwenzi wake wa jinsi alivyo.

ULEZI KWA VIJANA

Wakati wa ujana kamili matamanio huighilibu akili,

Endelea uk. 5

Mtume Mtukufu Muhammad s.a.w. ni mfano uliokamilika

Kutoka uk. 4

nayo husema; chupa ndani ya mto wa matamanio bila kuijali adhabu. Sasa sisi tutazame kama je Mtume s.a.w. aliwalea wanadamu (kukabiliana) na hali hii? Na tunapotafakari hufahamika kwamba alimlea baada ya yeye kuiona jadhba ya ujana wake.

Yeye alisema kuna mtu huoa kwa ajili ya kufuata nasaba, mwingine kwa kufuata mali, mwingine kwa kufuata urembo lakini nasaha yangu kwenu ni hii kwamba fungeni ndoa na yule ambaye asababishaye maendeleo ya maisha ya Akhera (Bukhari Kitabun Nikah, Babul ikfaai fid diin). Kwa sababu kama mtaoa kwa kuuona urembo, matendo yako yote katika uhai wako yatakuwa yanazunguka kwenye urembo, na yule aliyeoa mwanamke wa ukoo uliotukuka basi siku zote lengo lake litakuwa hivyo hivyo kwamba kwa hali yoyote ile lazima ajifanye mkubwa.

Yule mtu aliyeoa ndani ya familia inayofahamika kuwa ni yenye kuheshimika, basi juhudi yake yote itakuwa ni hii, iwe kwa udanganyifu, au kwa ulaghai, kadiri iwezekanavyo, kwamba ainasibishe familia yake na familia fulani ya kale. Miongoni mwa waislamu, Masayyid (Masharifu) ndio wanaofahamika kuwa ni waheshimika zaidi na kwa wahindu ni Wabrahman, na mtu wa aina hii, kwa vyovyote vile, daima atakuwa akijitahidi kujinasibisha na ukoo fulani wa kale ulioheshimika. Mhimili wa urembo daima huwa ni matamanio na ule wa mali na nasabu huwa ni wa udanganyifu, ulaghai na ulazimishaji.

Kuna kisa fulani maarufu cha kuchekesha cha wale wajinasibishao na koo zenye kuheshimika. Mtu fulani alienda kwenye mahakama fulani kwa ajili ya kutoa ushahidi na akajisema kuwa yeye anatokana na ukoo wa Masharifu. Upande wa pili ukalilalamikia jambo hilo. Mahakama ikamuuliza shahidi mwingine wa upande huo huo kwamba hali ya ukoo wa fulani ikoje? Yeye akasema huyu ni sharifu haswa. Baba yake tulikuwa tukimuona alikuwa ni mshona viatu, hivyo sisi sote ni mashahidi wa kuwa kwake sharifu kwani amejifanya kuwa sharifu mbele yetu.

Hivyo hili ni jambo la hovyo kabisa, kujiita tu kuwa ni sharifu kutafanya nini? Lakini wapo malaki ya watu wanaojibadili kaumu zao. Hivyo msingi wa maisha ya yule anayeoa kwa kufuata nasabu utakuwa ni wa uongo na ulaghai na msingi wa yule anayeoa kwa kufuata urembo huwa unakuwa ni wa matamanio. Lakini Mtume s.a.w. amesema kwamba kama leo hii nia yako si sahihi, sasa nini kitatokea siku zijazo. Hata msingi wa ndoa pia uufanye kuwa ni wa dini, kwa sura hii kazi zako zote mbili zitafanyika na vitendo vyako vitakuwa vinazunguka pembezoni mwa dini.

ULEZI KUHUSIANA NA NDOA

Baada ya kufanya uchaguzi, masharti ya ndoa huainishwa na kisha humo hutokea magomvi kwamba majukumu zaidi atwishwe mwanaume au mwanamke? Wa upande wa mume hutaka kuwatawala wa upande wa mke na wa upande wa mke hutaka kuwatawala wa upande wa mume. Lakini hapa pia Mtume s.a.w. yupo akisema lisikilizeni neno langu; Mungu Amemuumba mwanaume na mwanamke katika jinsi moja: Aliwaumbeni katika nafsi moja (4:2)

Hisia za wote wawili zi sawa na hamna tofauti yoyote kati ya (hisia zao) hizo. Kama vile mke awapendavyo wazazi wake, vivyo hivyo mume pia. Na ametoa utatuzi ambao kwa kuutekeleza wote wawili waweza kunufaika. Aliagiza kwamba muhurumiane kiundugu. (Bukhari Kitabul Adab bab fadhwli swiratwir rahim). Chini ya hukumu ya Mwenyezi Mungu zingatieni kuhurumiana kindugu na mseme kauli iliyonyooka;

na semeni usemi ulio sawa

Yaani msidanganyane. Kwa uchache yeye alitoa maagizo ya kina kuhusiana na ndoa ambayo kama niyaeleze basi hotuba hii itageuka kuwa hotuba ya ndoa. Kwa uchache ni hivi kwamba hata hapa pia Ametekeleza ulezi wake.

ULEZI WAKATI WA UJIO WA MKE

Halafu mke huja nyumbani na huo ni wakati ambao waweza kuelemewa na jadhba ya matamanio. Hapa pia Mtume s.a.w. akatokea na kusema kwanza itekeleze kazi yetu hii ndogo kwa kuomba dua. Matokeo ya uhusiano huu ni kwamba vitatokea vizazi vyenu vijavyo. Twaamini kwamba ninyi ni wema lakini yawezekana kuwa wazao wenu wakawa ni watukutu na hapo fujo ikaibuka duniani na ucha Mungu wenu mlioustawisha utafutika, hivyo mwombeni Allah dua kwamba matokeo ya kukutana kwenu yawe ni ya Ucha Mungu. (Bukhari Kitabud Daawaat, Bab ma yaquulu idhaa ataa ahlahu).

Huu ulikuwa ni wakati ambao matamanio yalikuwa yakitamani kupanda mbegu ya matamanio, lakini hali ya kiroho ilitaka mbegu ya kiroho ipandwe. Lakini Mtume s.a.w. akaja na kusema bila shaka pandeni mbegu ya matamanio, lakini pamoja na tamutamu ya kiroho.

ULEZI WA WAKATI AZALIWAPO MTOTO

Kisha watoto huzaliwa. Azaliwapo tu mtoto, papo kwa papo akalizingatia wazo la kumlea na kutoa maelezo ya kina kwa ajili ya malezi yake ambayo mfano wake haupatikani kwa kaumu nyingine yoyote ile. Agizo lake ni kwamba mara moja litajwe jina la Mwenyezi Mungu sikioni kwake. (Kanzul Ummaal jal. 16 uk. 599 Hadithi Nambari 46004, maktaba atturaathil islaamiyyi halb, chapa ya mwaka 1977).

Ingawa wakati huo mtoto huwa anaonekana kama kitu kisicho na uhai, lakini yeye s.a.w. akatoa agizo la kuutaja ukubwa wa Mwenyezi Mungu sikioni mwake na humo mna faida mbili. Kwanza ni kwamba jambo liingialo sikioni mwake kwa wakati huo huwa halipotei na pili ni kwamba wazazi wameelekezwa kwamba kama imetolewa hukumu ya kufanya malezi wakati ule ule wa kuzaliwa, basi jambo hilo litakuwa na umuhimu kiasi gani wakati atakapokua mkubwa.

HUKUMU YA MALEZI YA MTOTO

Wakati apatapo tu akili basi imeagizwa kwamba umuelimishe kiasi ya kwamba imesisitizwa hata katika kuwaelimisha pia watoto wa kike, kiasi ya kwamba akasema kuwa: Yule mtu mwenye mabinti wawili na kuwaelimisha na kuwapa malezi mazuri, basi makao yake yatakuwa ni Peponi. (Tirmidhi Abwaabul birri was swilati, babu maa jaa a fin nafakhati alal banaati wal akhwaati). Kana kwamba ameisema kuwa ni ya ulazima kiasi hiki kwamba amewalazimisha wazazi kufanya maandalizi hayo. Hivyo alisema :

Jiokoeni nafsi zenu na ahali zenu katika moto (At Tahriim : 7).

Humo mna elimu ya dhahiri na ya siri pia na wazazi wamelazimishwa zote hizo mbili na kusema kwamba wafundisheni watoto elimu zote mbili na kuwaepusha na Jahannam. Mradi wa Jahannam pia ni maradhi na umaskini n.k. ambavyo huzalika kutokana na ujahili. Na pia mradi wake Jahannam ya huko Akhera. Ilmuradi ametoa agizo la kuwaepusha watoto na kila aina ya Jahannam. Maadili mabaya pia ni Jahannam, kwa sababu watu huzichukia tabia mbaya. Hivyo aya hii ni ya mjumuisho na humo imetolewa hukumu ya kuwaepusha watoto na kila aina ya Jahannam na amesema kuwa ni lazima kwa Waislamu kwamba wawaangalie watoto katika hali za utotoni. Na akasema kuwa kama uharibufu upatikane humo basi mtaulizwa.

ULEZI KWA MAYATIMA

Halafu baadhi ya watoto hubakia mayatima. Kwa ajili yao pia alitoa maagizo kwamba mali zao zihifadhiwe:

Na wapeni yatima mali zao wala msibadilishe mazuri kwa mabaya, wala msile mali zao pamoja na mali zenu (4:3).

Kisha akasema ni namna gani zizingatiwe hisia zao. Mpango upi kwa elimu? Kwa uchache kuna maelezo ya kina kwa ajili ya utunzwaji wao. Kana kwamba hakuwaacha tu hivi hivi. Jambo hili halimo kabisa ndani ya dini zingine. Huko kama kuna kanuni za malezi ya watoto wao, lakini sio kwa ajili ya mayatima. Na kama zipo kwa ajili ya mayatima basi hazipo kwa ajili ya watoto wao. Lakini Mtume s.a.w. alizichukua zote na hakumuacha yeyote nje ya ulezi wake.

MWONGOZO KWA VIJANA

Baada ya hapo mwanadamu huwa kijana na pia Mtume s.a.w. anatoa hukumu zenye maelezo ya kina kuhusiana na ujana. Mathalan kuna uhuru kiasi gani katika jadhba. Wazazi watendewe vipi? Wazazi wawatendee vipi watoto wao walio vijana. Mtu mmoja alikuja kwa Mtume s.a.w. na kusema kuwa baba yangu amempa ndugu yangu farasi, lakini mimi hakunipa. Yeye s.a.w. akamwita na kusema; kama unao wasaa basi wape wote wawili na kama hauna basi mchukue huyo mmoja. (Bukhari Kitabul Hibati wa fadhwlihaa wa tahriidhwi ‘alayhaa, Babul hibati lil waladi wa Babul ish haad fil hibati).

Wakati hisia ya mwanamke na mwanaume inapokuwepo katika ujana, hata katika wakati huo pia, ametoa maagizo husika. Kuna mipaka gani kwa wasichana na kuna mipaka gani kwa wavulana. Wana uhuru gani katika masuala yao ya ndoa na wana mipaka ipi. Kuna uhusiano gani kati ya kaka na dada.

ULEZI KATIKA MASUALA YA KIDUNIA

Kisha, ametoa maagizo ya kina kuhusiana na kazi za kawaida wazifanyazo watu duniani. alisema kwamba haipaswi kufanya udanganyifu kwenye biashara, (Abu Daud, Kitaabul buyuu’i, bab fin nahyi ‘anil ghash). Ametoa maelezo tofauti ya mikopo ya muda mfupi na ile ya muda mrefu. Ametoa maelezo ya kina kuhusiana na uwekaji wa rehani na kanuni za mauzaji. Kwa uchache alitoa maagizo kwa ajili ya mahitajio yote haya. Mtu awapo mzee basi anatakiwa kutendewa vipi na watoto na akasema kwamba hata usiwaambie wazazi wako akh.

Wala usiwaambie hata Akh.. (16:24).

ULEZI WA ANAYEKARIBIA KUFA

Halafu kuna wakati pia wa mauti ambao ametoa maagizo yake na akasema kwamba huo ni wakati wa mwisho wa mwanadamu. Usiuharibu mwisho wa anayekaribia kufa kwa ajili ya maslahi yako madogo. Mpe fursa ya kujenga moyoni mapenzi ya Mwenyezi Mungu na ya kumuelekea. Watoto wako watakuwa na hali gani? Mke atafanya nini? Usipoteze nafasi hizi zenye thamani kwa kuyawazia maswali ya aina hii, bali uzisome aya za Kurani tukufu na sura Yasin mbele yake. (Sunan Abi Daud, Kitabul Janaiz, Babu Kiraat ‘indal Mayyiti). Baada ya hapo mfanye mpango wa kutatua matatizo yako mwenyewe na usiuharibu wakati wake wa mwisho kwa kuyataja taja (matatizo hayo).

Halafu akasema kama kuna mtu mwenye mali, basi anatakiwa aifanyie wasia tangu mwanzo

Mnalazimishwa mmoja wenu anapofikiwa na mauti, kama akiacha mali, kufanya wasia kwa wazazi, na jamaa sawa na sheria. Ndio wajibu kwa wamchao Mungu. (2:180), ili mambo haya yasimtishe wakati huo na alikuwa akiyatilia mkazo sana mambo haya kiasi ya kwamba sahabi fulani anasimulia kwamba: kila siku mimi nilikuwa ninalala na wasia ulioandikwa kwa kuuweka chini ya mto wangu. (Muslim Kitabul Waswiyyati, Bab waswiyyati rajuli maktuubatan ‘indahuu).

Na alitoa hukumu hii ili saa za mwisho za wenye kufariki zisiwe zinaharibika na wao waweze kuelekea kwa Mwenyezi Mungu. wakati huu ni wa kumwelekea Mwenyezi Mungu ili silsila hii iendelee pia katika maisha ya Akhera. Kama kuna yeyote ambaye wakati wa kufa atakuwa akiloloma; ee mke wangu, ee watoto wangu, basi atakapoamka mwelekeo wake utakuwa hivyo hivyo. Lakini kama wakati akifa atakuwa akisema Ewe Allah, basi wakati wa kufufuka pia mwelekeo wake utakuwa kwa Allah. Mfano wake ni wa aina hii kwamba kama mtoto alale huku akililia chapati, basi atakapoamka atakuwa bado anaikumbuka tu chapati. Kwa uchache Mtume s.a.w. hakughafilika na saa za mwisho za mwanadamu na akaagiza kwamba katika wakati huo Mwenyezi Mungu ahimidiwe na kutukuzwa.

Itaendelea toleo lijalo, Inshallah

Bustani ya Washairi

MSIKIVU ASIKIYE

1. Nianze kwa shahadatu, Allah nimuaminie
Asofanana na kitu, kingine tusujudie
Namuomba ithibatu, ukweli niutetee
Wa Isa kutumwa kwetu, msikivu asikie.
Yu mfu ajilalie, Yesu hatorudi katu
Hayo mdhaniyo nyie, si sunna ya Mola wetu.

2. Mpendwa Mtume wetu, rehema zimshukie
Swallallahu waswalatu, bishara atutajie
Kwamba zitafika kwetu, zama Isa atujie
Toka miongoni mwetu, msikivu asikie.
Yu mfu ajilalie, Yesu hatorudi katu
Hayo mdhaniyo nyie, si sunna ya Mola wetu.

3. Ila washika utatu, masheikh wawazingue
Na visivyo wakafutu, ukweli waupotoe
Eti yu mbingu ya tatu, Isa tumngojeae
Kumbe ufahamu butu, msikivu asikie.
Yu mfu ajilalie, Yesu hatorudi katu
Hayo mdhaniyo nyie, si sunna ya Mola wetu.

4. Si sunna ya Mola wetu, hayo mdhanio nyie
Kwamba amuweke mtu, mbinguni ajiishie
Asinywe, asile kitu, na hewa asipumue
Haupi nguvu utatu, msikivu asikie.
Yu mfu ajilalie, Yesu hatorudi katu
Hayo mdhaniyo nyie, si sunna ya Mola wetu.

5. Mungu hajafanya katu, wajinga wamzulie
Havunji Zake sunnatu, Mwenyewe Ajipangie
Kwamba maisha ya watu, ni ardhini yamee
Mwisho wawe amuwatu, msikivu asikie.
Yu mfu ajilalie, Yesu hatorudi katu
Hayo mdhaniyo nyie, si sunna ya Mola wetu.

6. Ameumba kila kitu, sheria akiwekee
Zao la dunia yetu, hapa pao libakie
Kwingineko sio kwetu, vipi tukajiishie
Ni kanuni madhubutu, msikivu asikie
Yu mfu ajilalie, Yesu hatorudi katu
Hayo mdhaniyo nyie, si sunna ya Mola wetu

7. Manabii ndugu zetu, hali zao kama sie
Hunywa na kuvila vitu, kuishi waendelee
Hawaukiuki utu, ardhi waikimbie,
Katamka Mola wetu, msikivu asikie.
Yu mfu ajilalie, Yesu hatorudi katu
Hayo mdhaniyo nyie, si sunna ya Mola wetu

8. Mitume vigezo kwetu, Tauhidi watetee
Sharia haithubutu, uungu iwadaie
Washindwapo kula kitu, ni lazima wajifie,
Aya zapiga upatu, msikivu asikie.
Yu mfu ajilalie, Yesu hatorudi katu
Hayo mdhaniyo nyie, si sunna ya Mola wetu

9. Walishapita wenzetu, kama hivi wadhanie
Eti alo samawatu, baadae awashukie
Yesu yeye mwema mtu, fumbo awafumbulie
"Yohana, Eliya kwetu, msikivu asikie."
Yu mfu ajilalie, Yesu hatorudi katu
Hayo mdhaniyo nyie, si sunna ya Mola wetu

10. Tajeni mmoja mtu, mfano mtutolee
Aloishi samawatu, akatumwa baadae
Tokea kuumbwa kwetu, vitabu mtusomee,
Hampati baraatu, msikivu asikie
Yu mfu ajilalie, Yesu hatorudi katu
Hayo mdhaniyo nyie, si sunna ya Mola wetu

11. Juu yake laanatu, Mola amzuliae
Tuwacheni utukutu, aya tuzifikirie
Tusafishe zote kutu, akilini zigandie
Ndio njia twayyibatu, msikivu asikie
Yu mfu ajilalie, Yesu hatorudi katu
Hayo mdhaniyo nyie, si sunna ya Mola wetu

12. Isa ni Mahdi wetu, Hadithi zifafanue
Wa Muhammadi umatu, azaliwe na akue
Si Israiliyatu, zama zao ziishie
Ahuishe dini yetu, msikivu asikie
Yu mfu ajilalie, Yesu hatorudi katu
Hayo mdhaniyo nyie, si sunna ya Mola wetu

13. Enyi nyoyo hasanatu, sikizeni mchungue
Katumwa Imamu wetu, kwa magoti tutambae
Kuchukua baiatu, Mitume waagizie
Ndio njia ya hayatu, msikivu asikie
Yu mfu ajilalie, Yesu hatorudi katu
Hayo mdhaniyo nyie, si sunna ya Mola wetu

14. Hapa nifike tamatu, huku nisisitizie
Ilonyooka swiratu, yeyote apendelee
Leo njia ni moja tu, Mahdi ampokee
Yesu hatorudi katu, msikivu asikie.
Yu mfu ajilalie, Yesu hatorudi katu
Msikivu asikie, si sunna ya Mola wetu

Abdulrahman M. Ame

USILE

1. Salaamu alaikumu, kwa wapenzi ndugu zangu
Nimeishika kalamu, niwakumbushe wenzangu
Haya mambo si adimu, nimengi tangu na tangu
Unapo kula vya kwangu, nafsiyo wadhulumu

2. Umeagizwa salamu, ili ufikishe kwangu
Ni salamu za muhimu, kutoka kwa somo yangu
Pesa zangu taslimu, ukazipiga kirungu
Unapokula vya kwangu, nafsiyo wadhulumu

3. Wajionea utamu, kumega mkate wangu
Hujui hiyo haramu, wewe kula jasho langu
Hiyo ulayo ni sumu, mbele ya Mwenyezi Mungu
Unapo kula vya kwangu, nafsiyo wadhulumu

4. Unanizibia gamu, uruke mithili pungu
Mbawazanguziwefumu,niwekamachunguchungu
Nitambaye humuhumu, nikitembea pindingu
Unapo kula vya kwangu, nafsiyo wadhulumu

5. Ufanyao ubahimu, sipendi moyoni mwangu
Hicho unachojikimu, maakuli ya wanangu
Kukupa sija azimu, wanipora langu fungu
Unapo kula vya kwangu, nafsiyo wadhulumu

6. Waninawisha na ndimu, macho yaone ukungu
Kwakuwa unakaimu, wanipiga na majungu
Huishi kunilaumu, kumbe ndo yako mizungu
Unapo kula vya kwangu, nafsiyo wadhulumu

7. Namuomba Muadhamu, mwenye ardhi na mbingu
Akupe ubinadamu, uwe na hofu yan Mungu
Usijitie wazimu, kukata yangu mikungu
Unapo kula vya kwangu, nafsiyo wadhulumu

8. Moyo usiwe mgumu, kama siki la mpingu
Kumbuka kuna hukumu, utakuja fungwa pingu
Utatiwa jihanamu, tena chini ya uvungu
Unapo kula vya kwangu, nafsiyo wadhulumu

9. Nimefikia khatimu, naenda nunua nyungu
Nami pia ninahamu, nizipike hizo dengu
Chonde nimetakalamu, usiwe miba za nungu
Unapo kula vya kwangu, nafsiyo wadhulumu

Mwl. Najat Fakim Saidi
Tanga - Mtiti Jamaat

PANYA

1. Zindukeni enyi watu, ngoja nikaliye sofa
Nisikize wanakwetu, niwapeni taarifa
Hanayo aibu katu, hata iwe kwenye dhifa
Panya ni mpenda sifa, hupita pita kwa watu

2. Dhamira atajwe jina, husahau hata kufa
Apate kujulikana, hata nyumba ya ghorofa
Hamuezi tulizana, atawatia ulofa
Panya ni mpenda sifa, nawala hajali kitu

3. Nguo atachanachana, ni mbaya zake kaifa
Anaudhi sanasana, pole ndugu bi Latifa
Nafaka akitafuna, hujitia na wadhifa
Panya ni mpenda sifa, siyo rafiki kwa watu

4. Nimejenga yangu nyumba, kwa nguvu na maarifa
Atakatakata kamba, ili alete maafa
Na mashimo atachimba, kusudi atie nyufa
Panya ni mpenda sifa, wala hafai kwa watu

5. Ana mtambaa panya, na bado haijafaa
Vurugu atazifanya, ataharibu vifaaa
Aking'ata na kunyonya, hukupulizia faa
Panya hanayo shufaa, huwatesa sana watu

6. Ndani mkitulizana, hii yake falsafa
Atapita pita sana, panya huyo huyo jafa
Ili mumtaje jina, yamjue mataifa
Panya ni mpenda sifa, hujipitisha kwa watu

7. Mwaka wa juzi na jana, nilipata zangu ofa
Safari ya kwenda China, na mengineyo masafa
Viza yangu kaichana, wivu wa zangu sharafa
Panya ni mpenda sifa, huwaharibia watu

8. Hakati sharubu zake, huzipakaza tu sifa
Husumbua wanawake, pia akina hanifa
Sipendi tabia zake, shahidi bwana halifa
Panya ni mpenda sifa, huwaudhi sana watu

9. Ningii mikia yao, raha yao sifa sifa
Utadhani nyumba yao, kwa bibi yangu sharifa
Wameharibu mazao, na mwenyewe alisafa
Panya ni mpenda sifa, hana huruma na watu

10. Ipo siku itafika, ninene na Mustafa
Alete sumu na paka, wakome yao misifa
Tuweze kusitirika, kwa uwezo wa Latifa
Panya ni mpenda sifa, huwahangaisha watu

11. Kaditama nimefika, nainuka kwenye sofa
Tisini zimeshafika, kama ningekuwa refa
Ya panya nimeandika, ninaifunga sahifa
Panya ni mpenda sifa, jihadhari enyi watu

Mwl. Najat Fakim said
Tanga – Mtiti Jamaat

1 Baiti ilo dhaifu, chini yake samawati
Hakuna ya kuturufu, ile yake ankabuti
Upepo huipa hofu, ikakosa hasanati
Ni nyumba ya ankabuti, maisha tuliyonayo

2 Tuwadogo jasiafu, wala hatuna wakati
Mara tumekuwa wafu, na jina letu maiti
Twajipaje utukufu?, nawauliza umati
Ni nyumba ya ankabuti, maisha tuliyonayo

Mahmood Hamsin Mubiru (Wamamba)

BURIANI Bi. RADHIA

1. Bismillahi Rabana,
Ni tukufu lako jina
Mfano wako hakuna
Wa milele na abadi

2. Wasalatu wasalamu
Zifike kwa Muadhamu
Muhammad Akramu
Alotumwa na Wadudi

3. Baada hizo salamu
Nina habari muhimu
Yalonipata ghulamu
Miye pamwe auladi

4. Msiba jama msiba
Kafariki wetu huba
Tulikula na kushiba
Ua letu la waridi

5. Msiba jama msiba
Kafariki mahabuba
Kwetu alikuwa tiba
Kuzituliza fuadi

6. Msiba jama msiba
Akina mama na baba
Imetukumba dhoruba
Na safari ni baidi

7. Msiba wangu shemeji
Amenipa mahitaji
Ya mawazo na ulaji
Yatetemeka jasadi

8. Tulenda wote Kibiti
Kanipa shamba katiti
Hadi nikapata hati
Shamba ni yake zawadi

9. Nazikumbuka bashasha
Na sururi isokwisha
Hai jamani maisha
Mara wapata baridi

10. Kwanza kazi za jamati
Hakupoteza wakati
Alizifanya kwa dhati
Usitadi na madadi

11. Mkonowe wa kutoa
Kushoto hadi kulia
Hakuweza limatia
Kutoa ni yake jadi

12. Alilonalo moyoni
Hakuficha asilani
Alitoa la rohoni
Kuitimiza miadi

13. Hakuna alo kamili
Ya Rabbi Moja Jalali
Mpe maziwa asali
Ya Rabbi Mola samadi

14. Pepo ina madaraja
Na mahali pa faraja
Mpatie wako mja
Karibu ya maseyidi

15. Tamati tumeridhia
Mapenzi yako Jalia
Na kwako tutarejea
Masikani yenye sudi

Na Mahmood Hamsini Mubiru (Wamamba)

Tukumbuke kule tulikotoka

Na Mwandishi wetu

Tarehe imeandikwa na wasomaji wamesoma kwa makini kabisa kwamba Jumuiyyaya Waislam wa Ahmadiyya, ilianzishwa mnamo mwaka 1889 na Hadhrat Sayidna Ahmad (as) kule Qadian India. Hata hivyo kwa msaada wa Allah ilisimikwa Afrika Mashariki mapema mwaka 1934 na Maulana Sheikh Mubaraka Ahmad (HA). Baada ya miaka miwili kupita, Sheikh alianzisha gazeti la Mapenzi ya Mungu mnamo mwaka 1936 na baadaye East African Times. Kisha utaratibu wa kujenga misikiti janibu mbalimbali wa ukanda huu ukaanzishwa na kuendelezwa.

Maulana Sheikh Mubarak alimuarifu Hadhrat Mirza Mahmood Ahmad (ra), Khalifa wa pili wa Seyidna Ahmad (as) kwamba Afrika Mashariki ni kubwa na yenye watu wengi wa mataifa na makabila tofauti. Sheikh alihitaji msaada maalum wa Khalifa Mtukufu. Aliomba wabashiri wengine zaidi waletwe kwa ajili ya Tabligh. Lakini kwa ukosefu wa fedha za kutosha, ombi hilo la Sheikh halikutekelezwa mara moja. Bali khalifa Mtukufu alichofanya ni kutuma wabashiri Afrika Mashariki kila ulipopatikana wasaa wa kufanya hivyo. Wabashiri walioletwa walipelekwa Uganda, Tanganyika na wengine kubakishwa nchini Kenya.

Katika harakati hizo za ujio wa Masheikh wa Kiahmadiyya, masheikh wakubwa wa kisuni wakaona hammadi! Wakastuka kuona kila nchi ya Afrika Mashariki Jumuiyya ya Ahmadiyya imeingia na watu kadhaa kujiunga nayo. Kulikuwapo na vikundi mbalimbali vya kiislamu vilijaribu kuizonga Ahmadiyya kwa hoja dhaifu sana. Majibu yalipotolewa yakawarejeshea fedheha na huzuni.

Mwaka 1953, Jumuiyya ya Ahmadiyya ilitowa tafsiri ya kwanza ya Qur'an Tukufu kwa lugha ya Kiswahili. Mashiekh wa kisuni wa



Sheikh Mubarak Ahmad (katikati) akiwa pamoja na Sheikh Amri Abedi kushotoni kwake pamoja na wabashiri wengine wa Ahmadiyya.

asili ya Afrika Mashariki na wa nje walichanganyikiwa vibaya mno. Wakajaribu kuwashawishi watu wasiisome ati watapotea! Ujinga bwana! Ujinga ni upofu wa kutoelewa mambo. Maombi ya Masheikh hao wa kisuni hayakupokewa na wafuasi wao. Bali wengi wao walisoma kwa hamu na shauku kubwa sana. Ukiachiya watu wa kawaida, lakini pia ilisomwa na machifu wa makabila mbalimbali wa Afrika Mashariki. Waislam kwa Wakristo waliisoma bila makengeza ya chuki. Kwa hili, mwanasiasa maarufu nchini Kenya na Afrika Mashariki kwa ujumla, Mzee Jomo Kenyata naye aliisoma Tafsiri hiyo. Yeye anakiri mwenyewe kwamba alipokuwa gerezani, wakati ule wa kikoloni wa kudai uhuru wa nchi hiyo, aliisoma zaidi ya mara mbili.

Masheikh wa Jumuiyya ya Ahmadiyya bado walikuwa wachache khasa baada ya kufumka upinzani. Mahitaji ya Wabashiri yaliongezeka mara dufu. Ndipo mpango wa kielimu ukapangwa. Sheikh Mubarak Ahmad akamshauri Khalifa Mtukufu wa pili umuhimu wa kuanzisha chuo cha Wabashiri ili wananchi watapomaliza na kuhitimu vizuri, waje washirikiane na Masheikh waliotoka Pakistan kwa shughuli za Tabligh. Sheikh Mubarak alishauri chuo hicho kiwe Tanganyika. Khalifa Mtukufu alikubali ushauri huo. Mnamo mwaka 1957, chuo cha Wabashiri wananchi kilianzishwa mjini Dar es salaam. Maulana Sheikh Kaluta Amri Abedi (Shahid) aliteuliwa kuwa Mkuu wa chuo akisaidiwa na Sheikh Ahmad Mataka Busra na Mwalimu B.K. Kheri.

Chuo kilijulikana kwa lakabu ya jina la AHMADIYYA MUSLIM MISSIONARY COLLEGE. Wakati chuo kinafunguliwa kilikuwa na tirimidhi wafuatao:-

1. Mbwana Shamte Nyengo - kutoka Rufiji sasa ni marehemu
2. Juma Abdullah Mpitakunza - kutoka Rufiji sasa ni marehemu
3. Omari Abdullah Matimbwa - kutoka Rufiji yu hai
4. Khamisi Sultani Wamwera - kutoka Rufiji yu hai
5. Athumani Mohammed Mkoka – kutoka Lindi sasa ni marehemu
6. Mahmood Abdullah Msham – kutoka Lindi sasa ni marehemu
7. Haruna Issa Kurunguja – kutoka Lindi sasa ni marehemu
8. Saidi Ally Shoo – Kutoka Moshi sasa ni marehemu
9. Adam Salmini Mushi – kutoka Moshi yu hai
10. Haruna Rashidi Bundala – kutoka Tabora yu hai
11. Shaabani John Komba – kutoka Songea
12. Mussa Omari Kizyara – kutoka Kigoma sasa ni marehemu

13. Hassani mohammed Ndambwe –kutoka D'Salaam yu hai, huyu alikuwa kiongozi wa wanafunzi hao.

Naam Maulana Sheikh Mubarak Ahmad akiwa Amir na Mbashiri Mkuu Afrika Mashariki, ilimbidi aketi Nairobi Kenya. Taarifa ya maendeleo ya chuo hiki yalikuwa yanamfikia kila wakati yanapohitajiwa naye alikuwa anayawakilisha kwa Khalifa Mtukufu wa pili.

Nisemetukwambamasomoya chuo yalikuwa yanaendeshwa kwenye sebule ya nyumba ya Jumuiyya Mnazi Mmoja sambamba na Masjid Salaam mjini Dar es salaam. Sebule hiyo hivi sasa ndiyo ofisi ya Makatibu mbalimbali wa Jumuiyya. Wanafunzi walikuwa wanalala Msikitini ambako kulipigwa patisheni kutenganisha nafasi hizo mbili.

Masomo ya darasani yalikuwa toka Jumatatu hadi yaumulkhamisi. Ijumaa ilikuwa siku ya mapumziko, ilikuwa siku ya Idi. Jumamosi na Jumapili zilikuwa siku mbili maalumu za Tabligh. Matirimidhi wote walikuwa wanaelekea mitaani kuzungumza na unasi mbalimbali. Pamoja na hayo, walikuwa wanauza vitabu vya Jumuiyya, magazeti ya Mapenzi ya Mungu na East African Times ambalo lilikuwa la lugha ya Kiingereza. Magazeti yote mawili yalikuwa yanachapishwa Nairobi Kenya na kufikishwa Tanganyika mjini Dar es salaam katika wakati muafaka. Hakuna mwezi ambao magazeti hayo hayakutoka. Kuchelewa kutoka kulikuwa nadra sana. Yalikuwa yanatolewa katika wakati muafaka sana kila mwezi.

Pamoja na hayo yote, pia palikuwapo na timu kabambe ya mpira wa miguu, iliitwa Ahmadiyya Young Timu. Iliundwa kwa shabaha ya mahubiri. Bali vijana waliweza kusawazisha viungo vyao kwa kuimarisha siha na afya yao pia. Kwa kweli timu ilipendwa sana na vijana ambao si Ahmadiyya. Ilikuwa timu ya utii na nidhamu ya hali ya juu. Vijana wasio Ahmadiyya, waliokuwa wanaishi karibu na Masjid Salaam waliathirika sana. Pamoja na kuingia kwenye timu, lakini baadhi yao walijiunga moja kwa moja katika Jumuiyya ya Ahmadiyya. Alhamdulillah.

Ni kweli kabisa kwamba Maulana Sheikh Kaluta Amri Abedi aliporuhusiwa na Khalifa Mtukufu wa Pili (ra) kwamba anaweza sasa kujiingiza rasmi kwenye uwanja wa siasa, hapo pia chuo hiki cha Ubashiri kilifikia tamati yake. Hata hivyo wakati huo vijana walikuwa wameiva barabara kwa Ubashiri na tabligh. Mwaka 1960, vijana baada ya kupokea mafunzo muruwa ya ubashiri kwa muda huo wa miaka minne, walikuwa tayari kufanya kazi za ubashiri wakishirikiana na wale waliotoka Pakistani. Basi wale waliofanya vyema zaidi kutoka chuoni hapo wakachukuliwa kwa kuitumikia Jumuiyya na wengine wao waliendelea na shughuli zao binafsi.

Kwa mazungumzo zaidi, Inshallah soma toleo lijalo.

Buriani Bi Radhia Amri Abedi Kaluta

Na Mahmood Hamsin
Mubiru – Dar es Salaam

Ulikuwa ni wakati wa joto jijini Dar es salaam. Nilikuwa nimekaa karibu ya mlango wa kuingilia Masjid salaam alipofungua mlango huo kijana aliyekuwa amelowa jasho. Alitoa salamu na kuniita pembeni, kwani wakati huo nilikuwa katibu wa elimu wa taifa wa Jamaat. Hali ilikuwa mbaya kuliko maelezo – alinieleza. Kesho ilikuwa ni siku ya mwisho ya kulipa ada ya kujiandikisha kwa ajili ya mitihani ya kidato cha nne. Hakuna nyumba aliyoiacha bila ya kubisha hodi na huko kote aliambulia patupu. Na kwa siku hiyo Ofisi za Jumuiyya zilikuwa zimefungwa na wahusika wote walikuwa wameelekea Morogoro.

Hadithi hiyo ilipokwisha, nikatambua ya kwamba mfuko wangu haukuwa na tofauti na wa yule kijana. Haraka nikapata wazo lililotokana na uzoefu. Taratibu niliongozana nae hadi Kaluta House alipokuwa Bi. Radhia akiongoza shule ya chekechea. Nilifika pale mara alipotuona akakimbilia dukani kutununulia soda na keki. Rohoni nikasema; 'angejua tunazihitaji pesa zote hizo'. Tukinywa soda nikaanza kutoa hadithi iliyotufanya tufike pale. Nilikuwa sijamaliza sentensi tatu, alipochomoka mithili ya mshale na kutuletea shilingi elfu thelathini ingawaje tulikuwa tumeomba ishirini. Nilipoanza kuanza kumshukuru alifanya kana kwamba hanisikii na akaleta mazungumzo minghairi ya hayo. Huyo ndio Bi. Radhia Kaluta Amri Abedi binti wa kwanza wa Sheikh Amri aliyezaliwa mwaka ule ule mwana Aliyeahidiwa alipotangaza kuwa 'ni mwana aliyeahidiwa' na msikiti wa kwanza wa Ahmadiyya huko Tabora ulipofunguliwa. Huo ni mwaka 1944.

Sidhani ya kwamba ni kutia chumvi kusema ya kwamba Radhia alikuwa na mkono wa kutoa. Na kila ukimtembelea hukosi kula vinono. Siku moja mimi na mdogo wake tulifika nyumbani kwake na nyama yote iliyokuwa kwenye chungu aliipakua ambayo ingeweza kufaa kesho yake. Lakini huyo ni Radhia aliyekuwa bingwa wa kukirimu wageni. Sheikh Inayatullah Ahmad aliyekuwa Mbashiri Mkuu nchini Tanzania alitembelea Moshi na kwenda



Bi Radhia Amri Abedi Kaluta (aliyekaa kwenye kiti) akiwa pamoja na kinamama wenzake kwenye moja ya mikutano ya Jalsa Salana nchini.

kumuona binti yake Radhia aliyekuwa anafanya kazi mjini Moshi. Hali haikuwa nzuri pale nyumbani na jasho jembamba lilikuwa linamtoka Bi. Radhia licha ya baridi ile ya Moshi. Sheikh Inayatullah Ahmad aligundua mahangaiko hayo na kumtuliza binti yake kwa kumwambia apike chochote kilichokuwepo.

Bi. Radhia aliwaheshimu sana Wabashiri. Bw. Mburulo alipotaka kumuoa, alimwambia akaombe idhini kutoka kwa Sheikh Inayatullah Ahmad ambaye siku zote alimchukua kuwa baba yake.

Umewahi kusikia 'zege halilali' na ndio ulikuwa mwenendo wa Bi. Radhia akipewa kazi ya Jamaat. Bw. Mohammed Saidi Lone aliniomba mimi na Bi. Radhia tutafsiri kwa Kiswahili kitabu cha Maulana Abul Ata kiitwacho Yesu Msalabani. Tulipokwisha maliza kutafsiri tukampa mtu wa tatu aipitie Bi. Tahira Swaleh Mbaruku. Nae alipokwisha maliza akaturejeshea. Mimi nilikaa nacho siku mbili tatu. Lakini kilipofika kwa Bi. Radhia aliupitia mswadahuo kwa kasi ya ajabu na usiku nilimuona anauleta ili kutimiza ile hadithi ya 'Zege halilali'.

Kubweteka haukuwa utamaduni wake. Na awe na fedha hana fedha ilikuwa vigumu kumtambua. Licha ya hali ya kuridhisha ya watoto wake alipata shamba huko Kibiti na kuanza kulima. Tuliwahi kwenda sote shambani kwake alikokuwa amejenga nyumba yake ndogo nzuri aliyeipa jina 'White house'. Kufika haraka haraka akatafuta kuni na kusonga ugali. Mara hiyo akaenda kuwaita majirani ili tupate chakula kwa pamoja. Wasaidizi wake walimpenda kwani hukuweza kutambua kuwa ni nani alikuwa mwenye shamba na nani alikuwa mtumishi. Basi kivumbi alipovuna. Majirani wote hawakukosa mgao, usiwataje wadogo zake. Kwa hakika kilele cha furaha yake ilikuwa ni kutoa.

Wajumbe wa Majlis Amila hapa Dar es salaam wanakumbuka walivyokuwa wanasubiri kwa hamu siku ya kikao cha Majlis Amila. Ambapo Bi. Radhia bingwa wa mapishi aina aina alipowatengenezea mithili ya boflo iliyowekwa mayai na vingine ambavyo ni vigumu kuvikumbuka.

Sheikh Khalfan Kiumbe wa Ujiji Kigoma alionesha dalili zote za uhasama wa hali ya juu kuhusu Jumuiyya ya Ahmadiyya. Alitoa matusi na kuwaamuru wafuasi wake wamwagie mchanga na kumzomea Sheikh Kaluta Amri Abedi. Na kosa kubwa la Sheikh Amri ni kwamba alieleza kuwa Mtukufu Mtume Muhammad (saw) ni Rehema kwa watu wote, sababu ya kuumbwa kwa dunia, mbora wa viumbe, aliyeleta sheria kamili na katu haitakuja sheria ya kuipiku aliyoileta. Isipokuwa si nabii wa mwisho. Mlango huo upo wazi kwa anayepata cheo hicho kutokana na kuwa mfuasi mtiifu na mnyenyekevu wa Mtukufu Mtume Muhammad (saw). Wazo hilo liliibua kitimtim na tufani kwenye kikombe cha chai. Sheikh Kiumbe akapita huko na kule akitangaza ukafiri wa Sheikh Amri na kusisitiza kuwa kapotea na Sheikh Kiumbe akasisitiza ya kwamba upotofu wa Sheikh Amri umezidi pale alipodiriki kutangaza ya kwamba Nabii Isa amefariki na kuzikwa Srinagal nchini India. Uhasama ulikuwa ni mkubwa na uliopitiliza. Lakini tizama binti aliyefunzwa na Sheikh Amri. Miaka mingi baadae katika hali ya udhalili na unyonge Sheikh Khalfan Kiumbe alifika tawi la Benki ya Taifa huko Kigoma akiongozwa na mtu kwani uwezo wa kusimama sawasawa hakuwa nao. Watu walikuwa wengi na hakukuwa na yeyote aliyemjali kwa kumpa fursa ya kwenda kuhudumiwa kwanza. Bi. Radhia ambaye alikuwa mfanyakazi wa Benki hiyo alipomuona tu haraka akamtoa kwenye mstari na kumpa huduma haraka. Alipokwisha muhudumia akamuuliza; 'Baba unanifahamu?' Sheikh Kiumbe akamtazama na akajibu; 'Mama sikufahamu'. Bi. Radhia akamwambia; 'Mimi ni binti wa Sheikh Amri'. Sheikh Kiumbe akadondosha machozi. Kwa njia iliyo nzuri Bi. Radhia akawa amefikisha ujumbe wa 'Mapenzi kwa wote bila chuki kwa yeyote'.

Watafiti juu ya maisha ya Sheikh Kaluta Amri Abedi walitulizwa kiu yao kwa maelezo ya kina ya Bi. Radhia kuhusu Sheikh Amri. Ni dhahiri ya kwamba yeye alimfahamu vilivyo na mengi ya matukio yanayosimuliwa katika sheria za kutunga mashairi na Diwani ya Amri kwa njia moja ama nyingine yanamhusu Bi. Radhia. Nakumbuka alipokuwa akisoma Diwani ya Sheikh Amri kila lipofika kwenye shairi la 'Kina ningali mtini, sina mama kunilea' –machozi yalikuwa yanamtoka. Profesa Mugyabuso Mlokozi alifunga safari hadi Ujiji kwenda kuonana na Bi. Radhia na mwisho wa mazungumzo naye alikiri ya kwamba Bi. Radhia ni Kamusi kuhusu maisha ya Sheikh Amri Abedi. Elimu hii juu ya Sheikh Amri aliitoa kwa furaha bila vikwazo. Sisi ambao tunajaribu kuandika maisha juu ya baadhi ya washairi tunafahamu matatizo tunayopambana nayo kutoka na ndugu za washairi hao kututoa ushirikiano unaofaa. Hapana shaka maji katika kisima kuhusu Sheikh Amri yamepungua kutokana na kuondoka kwa Bi. Radhia.

Siku moja nilikutana nae akiwa katika haraka na nikamuuliza alikuwa anakwenda wapi? Alinieleza kuwa alikuwa anakwenda Msikitini kulipa mchango. Jambo la utoaji wa michango alilipa kipaumbele na hakusita kutukumbusha juu ya umuhimu wa kutoa michango.

Asubuhi alifika nyumbani, nilikuwa katika chumba changu cha kujisomea. Aliniambia kuwa; 'Bwana leo nimekuja nina ombi kubwa'. Nilitulia kumsikiliza. Aliniambia kuwa; 'Naomba niende na mdogo wangu hija'. Nilitabasamu na kusema; 'Allah aibariki hija yenu'. Tizama heshima aliyokuwa nayo na alivyoelewa mafunzo ya Islam.

Habari hizi zimeelezwa kwa nia moja. Asaa tukajifunza jambo kutoka katika maisha ya Bi. Radhia Kaluta.

1. Hasara kubwa fahamu,
   si kupoteza fulusi
   Ingawa kitu adhimu,
   kwa sisi sote unasi
   Kipo kilo akramu,
   kinachozidi ukwasi
   Roho iliyoelewa,
   hiyo baraka kabiri

2. Roho iso na elimu,
   kumtambua kudusi
   Ni hasara ilotimu,
   nyumba yake ibilisi
   Hasara kwa binadamu,
   kudumu kwenye uasi
   Hasara thamma hasara,
   roho iliyopotea

3. Na jicho lisilotimu,
   kuiona adharusi
   Kuona yalo haramu,
   yaletayo wasiwasi
   Kwa sisi binaadamu,
   maizi hiyo nuhusi
   Hasara kubwa ajabu,
   kwa sisi tulo unasi

Ibada na taratibu za Mazishi ya Kiislam

Na Syed A. Majid Shah na B. K Ahmad

(Imetafsiriwa kutoka gazeti la Ahmadiyya Gazzete Canada)

Inapoonekana kifo kinakaribia, usomaji wa sura Yasini (Sura ya 36 ya Kurani Tukufu) unashauriwa.

Maudhui yaliyoelezwa ndani ya sura hii ni yenye asili ya kuondoa maumivu kwa anayefikwa na umauti au kukata roho na kumpa utulivu wa nafsi.

Kwa aliyopo karibu na mtu anayekaribia kukata roho anapaswa kusoma kwa sauti ya chini lakini yenye kusikika ***Takbira*** na ***Kalima shahada***. Mtu anapokuwa amekufa, watu wote waliopo na watakaopata habari ya kifo wanapaswa kusoma dua ifuatayo:-

﴿ إِنَّا لِلَّهِ وَإِنَّآ إِلَيْهِ رَٰجِعُونَ ﴾

"Inna lillaahi wa inna ilaihi raajiuun" – yaani; Hakika sisi ni wa Mwenyezi Mungu, na kwake tutarejea.

Macho ya marehemu yanapaswa kufumbwa kwa kutumia viganja vya mikono na nguo inapaswa kufungwa kwa kuzungushwa baina ya kichwa na kidevu ili kuacha mdomo katika hai ya kufumba. Ufanyaji wa ibada na taratibu za mazishi (kuosha mwili, kuvisha sanda, kusalia na kuzika) ni lazima kwa waaminio wote, lakini huchukuliwa kama "*Faradhi kifaiyya*". Hii ni kusema, kama watu watatu au zaidi watashughulikia ibada na taratibu za mazishi, wengine wote watahesabiwa wameondokana na dhambi, vinginevyo ni lazima kwa kila mtu. Kama katika jamii hakuna anayeshughulikia ibada na taratibu za mazishi ya Muislam, jamii hiyo yote itachukuliwa kuwa ni yenye dhambi kwa kutotunza mwili huo. Hivyo ni muhimu kwa kila mmoja kufahamu mambo ya msingi ili kutekeleza jukumu hilo.

KUUOSHA MWILI WA MAREHEMU.

Maji mazuri na masafi ya uvuguvugu yanapaswa kutumika kuosha mwili wa marehemu. Desturi ya mtukufu mtume (saw) ilikuwa kuweka majani beri (aina ya mti wa mjojoba) katika maji yanayotumika kuoshea mwili wa marehemu. Kama majani ya beri hakuma, kiasi kidogo cha kemikali / dawa inayozuia kukua kwa bakteria (kuondoa harufu) kinaweza kutumika. Sehemu za siri za marehemu zinapaswa kuoshwa kwanza, kufuatia sehemu zote zinazooshwa wakati wa udhu kama vile viganja, uso, mikono, viwiko n.k. Haihitajiki kutia maji mdomoni au puani.

Kisha sehemu zote za mwili zinapaswa kuoshwa mara tatu, kwa kuanza upande wa kulia na baadae upande wa kushoto. Sehemu za siri za marehemu zinapaswa kuwa zimefunikwa kwa nguo wakati wote huo.

Ni wanaume pekee wanaweza kuosha mwili wa mwanaume na wanawake mwili wa mwanamke. Lakini kama wanawake hawapo, mume anaweza kuosha mwili wa mkewe na kinyume chake.

KUVISHA SANDA (KUKAFINI) AU KUUVISHA MWILI.

Baada ya mwili kuoshwa na kukaushwa, hatua inayofuata ni kuuvisha sanda, ambayo huhusisha kuuvisha mwili nguo nyeupe kwa utaratibu maalum. (yaani vipande vitatu kwa wanaume na vipande vitano kwa wanawake). Sanda (kafan) inapaswa kuwa nguo nyeupe isiyoshonwa na rahisi (isiyo na gharama au yenye bei nafuu). Kwa wanaume, sanda inakuwa na vipande vitatu vya nguo:-

1. Shuka ya chini, kipande cha nguo kinachofunika kikamilifu sehemu za chini za mwili (mbele na nyuma) kama sketi.
2. Shuka ya juu, kipande cha nguo kinachofunika sehemu za juu za mwili kama shati.
3. Shuka kubwa, kipande cha nguo ambacho kinafunika mwili wote kuanzia kichwani mpaka miguuni na inakuwa ndefu na pana kiasi cha kutosha kufunga sehemu zake za juu na chini kwa kutumia mkanda au kamba iliyotengenezwa kwa kutumia nguo hiyo hiyo.

Vipande hivi vyote vinakatwa mapema na kuwekwa tayari ili kurahisisha uvishaji pindi mwili unapolazwa juu yake. Kwa wanawake, ziada ya vipande viwili vya nguo hutumika, kimoja kwa ajili ya kifua na kingine kwa ajili ya kichwa.

Mwili wa Shahidi (aliyeuawa katika njia ya Mwenyezi Mungu) hauhitaji kuoshwa au kuvishwa sanda na unapaswa kuzikwa na nguo zake alizozivaa wakati wa kifo chake.

SALA YA JENEZA

Baada ya mwili kuoshwa na kuvishwa sanda, unapaswa kuwekwa kwenye jeneza na kupelekwa mahala ambapo sala ya jeneza itasaliwa. Sala ya jeneza husaliwa katika mkusanyiko wa kutosha, ndani au sehemu ya wazi (nje).

Jeneza huwekwa mbele ya Imamu hivyo kwamba uso wa marehemu huelekezwa upande wa Ka'abah (kibla). Watu wote waliyopo kwa ajili ya sala ya jeneza wanapaswa kujipanga katika safu zenye idadi ya witri nyuma ya Imam. Imam huanza sala kwa kutamka "Allah Akbar" (Mungu ni Mkubwa) kwa sauti wakati akipandisha (akinyanyua) mikono yake masikioni. Maamuma hutamka vivyo hivyo kwa sauti ya chini (kimoyomoyo). Baadae Imam anasoma kwa kimya Thanaa na Sura Fatiha. Maamuma nao hutamka vivyo hivyo kimoyomoyo. Imam hutamka tena "Allah Akbar" bila kupandisha / kuinua mikono yake. Wafuasi (Maamuma) hutamka vivyo hivyo kwa sauti ya chini bila kupandisha mikono yao. Jamaa (wanaosali wote) yote hutamka Durud Sharif (Sala ya Mtume) kimoyomoyo. Baada ya Durud Sharif, Imam anatamka tena "Allah Akbar" kwa mara ya tatu na kila mmoja husoma maombi maalum kwa ajili ya marehemu kimoyomoyo. (Tazama maombi chini). Imam anatamka tena "Allah Akbar" kwa mara ya nne na ya mwisho na kugeuza uso wake upande wa kulia na kusema "Assalam Alaikum warahmatullah" (Amani na baraka za Allah ziwe juu yako). Kisha anarudisha uso wake upande wa kushoto na kurudia maneno yaleyale, kuashiria mwisho wa sala. Wafuasi / Maamuma wanafanya vivyo hivyo na kurudia kimoyomoyo maneno "Assalam Alaikum warahmatullah" kwakugeuza nyuso zao kulia na kushoto.

Hakuna rukuu au sujuda katika sala ya jeneza. Sala ya jeneza ghaib (sala ya jeneza kwa mtu aliyezikwa) inaweza kusaliwa kwa mtu aliyefariki hususani kwa mtu / watu maarufu au mashuhuri au pale ambapo waislam wachache walikuwepo wakati wa sala ya jeneza iliposaliwa kwa mara ya kwanza. Hata hivyo kusali sala ya jeneza ghaib isichukuliwe kuwa ni desturi au utaratibu wa kawaida. Kama aliyekufa ni mkubwa mwanamume au mwanamke dua ifuatayo huombwa:-

اَللّٰهُمَّ اغْفِرْ لِحَيِّنَا وَمَيِّتِنَا وَشَاهِدِنَا وَغَائِبِنَا
وَصَغِيرِنَا وَكَبِيرِنَا وَذَكَرِنَا وَأُنْثَانَا
اَللّٰهُمَّ مَنْ أَحْيَيْتَهُ مِنَّا فَأَحْيِهِ عَلَى الْإِسْلَامِ
وَمَنْ تَوَفَّيْتَهُ مِنَّا فَتَوَفَّهُ عَلَى الْإِيمَانِ
اَللّٰهُمَّ لَا تَحْرِمْنَا اَجْرَهُ وَلَا تَفْتِنَّا بَعْدَهُ

Matamshi: ***Allahummaghfir lihayyina wa mayyitina, wa shaahidina wa ghaibina, wa saghirina wa kabirina, wa dha- karina wa unthana. Allahumma, man ahyaitahuu minnaa fa-ahyihii alal-Islam; wa man tawaffaitahuu minnaa fatawaf- fahuu alal-Iman. Allahumma la tahrimna ajrahu wala taftinna ba'dah.***

Tafsiri: E Allah, wasamehe walio hai kati yetu na waliokufa, na waliohudhuria na wasioweza kuhudhuria, na wadogo wetu na wakubwa wetu, na wanaume wetu na wanawake wetu. Ee Allah, usitunyime ujira wake wala usitutie majaribio baada yake.

Zingatia: **Iwapo maiti ni ya mwanamke msitari wa mwisho wa dua utasomeka:**

اَللّٰهُمَّ لَا تَحْرِمْنَا اَجْرَهَا وَلَا تَفْتِنَّا بَعْدَهَا

Allahumma la tahrimna ajraha wala taftinna ba'daha.

Sala ya jeneza kwa mtoto wa kiume.

Dua ifuatayo husomwa badala ya iliyotajwa awali.

اَللّٰهُمَّ اجْعَلْهُ لَنَا سَلَفًا وَفَرَطًا وَاجْعَلْهُ لَنَا أَجْرًا وَذُخْرًا
وَاجْعَلْهُ لَنَا شَافِعًا وَمُشَفَّعًا

Matamshi: ***Allahummaj'alhu lana salafan wa faratan, waj'alhu lana ajiran wa dhukhran, waj'alhu lana shafian wa mushaffa-an***

Tafsiri: Ee Allah, umfanye mtangulizi wetu, na umjaalie awe ujira na akiba kwetu, na umjaalie kuwa mwenye kutuombea na ambaye maombi yake hupokelewa.

Sala ya jeneza kwa mtoto wa kike

Dua ifuatayo huombwa badala ya zilizotajwa juu.

اَللّٰهُمَّ اجْعَلْهَا لَنَا سَلَفًا وَفَرَطًا وَاجْعَلْهَا لَنَا أَجْرًا وَذُخْرًا
وَاجْعَلْهَا لَنَا شَافِعَةً وَمُشَفَّعَةً

Matamshi: ***Allahummaj'alha lana salafan wa faratran, wa dhukhran wa ajran, wa shafiatan wa mushaffa-atan.***

Tafsiri: Ee Allah, mjaalie awe mtangulizi wetu, na akiba na ujira kwetu, na mwenye kutuombea na mwenye kupokelewa maombi yake.

MAZISHI

Baada ya sala ya jeneza, mwili unapaswa kupelekwa makaburini (maziarani au mavani) kwa ajili ya mazishi bila kuchelewa. Waombolezaji wote wanapaswa kusindikiza mwili makaburini. Waombolezaji wote wanafuata msafara wa mazishi wanapaswa kuendelea kumkumbuka Allah (Zikr-e-llahi) sambamba na kumuombea msamaha marehemu kwa sauti ya chini.

Kaburi linaweza kuandaliwa kama vile shimo lililochimbwa likiwa na mwana wa ndani kwa ajili ya kulaza mwili au linaweza kuwa shimo lililochimbwa – bila mwana wa ndani. Ni muhimu kwa kaburi kuwa pana na lenye nafasi. Katika hali ya kuzidi kiasi (dharura) miili zaidi ya mmoja inaweza kuzikwa kwenye kaburi moja. Mwili unapaswa kuteremshwa kaburini kwa uangalifu na umakini mkubwa. Mwili unapokuwa unateremshwa kaburini, shuka iliyofunikwa inapaswa kufunguliwa (kulegezwa) kidogo sehemu ya wazi na uso unasogezwa kidogo kuelekea upande wa Ka'abah (kibla). Mwili unapokuwa unateremshwa ardhini, dua ifuatayo husomwa:-

بِسْمِ اللّٰهِ وَ بِاللّٰهِ عَلَى مِلَّةِ رَسُولِ اللّٰهِ صَلَّى اللّٰهُ عَلَيْهِ وَ سَلَّم

Matamshi: ***Bismillahi, Wabillahi, 'alaa millati Rasulillaahi s.a.w.***

Tafsiri: (Twamzika) kwa jina la Allah, na kwa baraka za Al- lah, juu ya desturi ya Mjumbe wa Allah s.a.w.

Pale jeneza (mwili) linapofunikwa na udongo mwepesi (mchache), dua ifuatayo husomwa:-

﴿ مِنْهَا خَلَقْنَٰكُمْ وَفِيهَا نُعِيدُكُمْ وَمِنْهَا نُخْرِجُكُمْ تَارَةً أُخْرَىٰ ﴾

Endelea uk. 9

Uchamungu ndio msingi wa maendeleo yote

Kutoka uk. 12

ya kufanikiwa kwenye maisha haya ya dunia na yake yajayo, na msingi huo ni kwamba tushughulike zaidi na maisha yajayo. Kanuni hii huyapamba maisha ya mtu kwenye dunia hii na ijayo. Kwa ajili ya kujitayarisha na maisha yajayo ni lazima mtu aanzie hapa tena sasa.

Aya iliyotangulia 59:19 ni moja ya aya inayosomwa wakati wa hotuba ya ndoa. Ni aya ya mwisho kwenye hotuba ya ndoa. Katika hotuba ya ndoa Mwenyezi Mungu anatukumbusha kuzingatia masuala mbalimbali, kujali mahusiano ya kifamilia, kushika uaminifu na ukweli ili kumuwezesha mtu kutenda matendo mema pamoja na kutimiza haki zote za udugu. Pia tunakumbushwa kushika amri za Mwenyezi Mungu na maagizo ya mtukufu Mtume s.a.w. na pia msisitizo huwekwa kwamba iwapo mtu atayaweka maisha yajayo mbele ya macho yake kila wakati, basi mtu huyo pia ataziweka amri za Mungu na maagizo ya Mtukufu Mtume s.a.w. mbele ya macho yake muda wote.

Kuna amri nyingi za Mwenyezi Mungu na maagizo Mtume Wake ambayo yanasaidia kuyafanya maisha ya familia au ya kindoa kuwa mazuri. Maisha ya mtu kifamilia yanakuwa kama pepo na pia mtu anapata tumaini jema la maisha yajayo kutokana na matendo yake kuwa mazuri. Na jambo hili haliishii kwenye maisha ya mtu mwenyewe tu, bali Baraka zake hufika mbali na watoto wake nao huwa warithi wa Baraka hizo.

Iwapo familia zinazoyaharibu maisha yao ya majumbani kwa vijambo vidogo vidogo tu wangezingatia amri za Mwenyezi Mungu na kuzitekeleza, sio tu kwamba wanakuwa walinzi wa familia zenye amani, bali pia wanayachonga maisha ya watoto wao kuwa mazuri. Familia ambazo zinayaharibu maisha ya nyumba zao kwa mambo madogo madogo ya kidunia zizingatie sana juu ya hili. Kizazi chenu kijacho sio tu cha kwenu peke yenu, bali pia ni hazina kwa ajili ya Jumuiya na taifa kwa ujumla. Hivyo ni wajibu wa wazazi kuwaonesha watoto wao njia iliyo sawa hili litawezekana tu iwapo wazazi wenyewe watashika amri za Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Katika aya hii Mwenyezi Mungu amemkumbusha kila mwaminio juu ya ukweli huu.

Kuna matukio mengi kwenye maisha yetu ambapo tunajisahau kushika utawa na kujali maisha yajayo. Kwa mbali tunatoa umuhimu zaidi juu ya dunia kuliko Mwenyezi Mungu. Kutokana na udhaifu wetu huu na kushindwa tunaiangamiza khatima yetu kwenye maisha haya na kuyasahau maisha yetu yajayo.

Huzur, akasema kwamba muumini anatakiwa kwanza atafakari juu ya matokeo ya kila jambo kabla hajaanza kulitenda. Wakati anapokasirika, mtu anaonesha tabia mbaya na kutoa matusi. Lakini tunatakiwa tufikiri kwanza juu ya madhara ya jambo hili. Kufikiria kwanza juu ya madhara / matokeo ya tendo lolote kabla ya kulifanya humuongoza mtu kushika njia ya utawa. Makosa yote au maovu huzalika kutokana na ukweli huu kwamba tunakuwa na shetani kwenye mawazo yetu na hapo tunafanya lolote tunalowaza tulifanye bila ya kufikiria madhara ya jambo hilo. Hapa hawakusudiwi wale ambao ni wazoefu kwenye kutenda maovu, au wale ambao hawajiwezi kabisa katika kujidhibiti kimatendo. Bali hapa wanakusudiwa wale wenye imani.

Hadhrat Khalifatul Masih I r.a. aliwahi kusema mtu anatakiwa awe na imani thabiti kwamba Mwenyezi Mungu anamuona na anamuangalia kwa kila akifanyacho. Iwapo mtu anaamini kwamba yule anayekitawala na kukiongoza kila kitu na ambaye pia ni mwelewa wa kila kitu na anazo habari za kila jambo anamuona katika kila kitendo chake kiovu, kisicho na maana na chenye kuchukiza, na kwamba atamuadhibu kwa hilo, bila shaka mtu anaweza kuiepuka adhabu hiyo kwa kushika njia njema. Hii ndio imani ambayo kila mmoja wetu aikuze ndani yake. Iwapo mtu hatekelezi kwa umakini jambo lake lolote hata katika mambo ya kidunia, bila shaka hawezi kupata malipo yafaayo kwa jambo hilo au kwa neno zima jambo lake haliwezi kukubalika na yoyote. Aya hii ya 59:19 ambayo inamkumbusha mtu juu ya kuijali kesho yake bila shaka inayo maana na falsafa kubwa zaidi.

Tuna haja ya lazima ya kukuza ndani yetu imani hii kwamba Mwenyezi Mungu anatuaona na analiangalia kila tendo letu, na pia kuna haja ya kukuza ndani yetu imani hii kwamba aina yoyote ya kughushi (kutokuwa mwaminifu), hata kuwe kudogo kiasi gani tutakakokuona, au uzembe wowote, au kutokutimiza majukumu yetu ni jambo linalochukiza mbele ya Mwenyezi Mungu. Kwa kuwataka waaminio wangalie kile wanachokitanguliza kwa ajili ya kesho yao, Mwenyezi Mungu alikusudia kwamba tushike utawa katika kila jambo letu, liwe ni la kifamilia, la kibiashara au liwe ni jambo la kitaifa au hata kimataifa. Mtu (wa kidunia) anaweza kudhani kwamba mambo ya kidunia hayana muunganiko na imani, lakini mwaminio anaamrishwa kushika utawa katika kila kitu.

Baadhi ya nyakati watu huchukua maamuzi ili kujikinga na hasara ya kidunia, lakini ikumbukwe kwamba hatua yoyote atakayochukua mtu ambayo ndani yake inaingiza kujipatia manufaa ya kidunia kwa njia ya kughushi au kuhadaa jambo hilo linamweka mtu mbali na dini na imani. Kidogo kidogo mtu anakuwa mbali na dini na Mungu. Hivyo mtu anatakiwa aweke mbele yake madhara ya kila akifanyacho kwani Mwenyezi Mungu anaangalia kila tendo tulifanyalo.

Kwa ajili ya hili mtu hahitaji apate dodoso kutoka kwenye taasisi / tanzeem yoyote. Kwa hakika kila mmoja wetu anatakiwa ajitathmini mwenyewe katika ngazi yake binafsi. Iwapo tunafanya kitu chochote kwa ajili ya kupata radhi za Mwenyezi Mungu basi tutapata malipo mara mbili. Lakini kama lengo letu la kufanya jambo fulani sio sawa basi tuelewe kwamba tunaweza kushikwa na adhabu ya Mwenyezi Mungu.

Iwapo kila mmoja wetu atatekeleza wajibu wake kwa kuzingatia haya, hali ya uchamungu ndani ya Jumuiya kwa ujumla itaongezeka na itaonekana bayana kwa jamii zingine. Hakutohitajika sana uingiliaji wa Idara ya Tarbiyyat au ya Umur Aamma au idara nyingine yoyote. Hivyo kila mmoja wetu ajiangalie yeye mwenyewe kwa kudumu na kila mmoja wetu awekeze juhudi kubwa na maalum kujilinda na mashambulizi ya kishetani.

Mwisho.

Ibada na taratibu za Mazishi ya Kiislam

Kutoka uk. 9

Matamshi: ***Minha khalaqnaakum wa fiihaa nuidukum wa minha nukhrijukum taaratan ukhra.***

Tafsiri: Tuliwaumbeni kutoka humo na mle ndani yake Tutawarudisheni na kutoka humo Tutawatoeni mara nyingine.

Ilikuwa ni desturi ya Mtukufu Mtume (saw) kufanya kaburi limenyanyuka kidogo kutoka usawa wa ardhi. Mazishi yanapomalizika maombi mafupi ya pamoja na ya kimoyomoyo kwa kuinua mikono huombwa kwa ajili ya kumuombea msamaha (maghofira) marehemu. Waombolezaji wanatakiwa kuondoka makaburini huku wakisoma dua ifuatayo kimoyomoyo:

اَلسَّلَامُ عَلَيْكُمْ وإِنَّا
إِنْ شَاءَ اَللّٰهُ بِكُمْ لَلَاحِقُونَ

Matamshi: ***Assalaamu Alaikum. Wa innaa Insha-Allahu bikum lalaahiquun.***

Tafsiri: Salamu iwe kwenu. Nasi Mungu Akijaalia, tutakutana nanyi.

Rambirambi (Mkono wa pole)

Wanajamii (Ndugu, jamaa na marafiki) wanapaswa kutoa rambirambi kwa ndugu wa marehemu. Inashauriwa kwamba watu wa karibu na wapendwa (wa familia) au majirani wawapatie chakula familia ya marehemu kwa siku tatu. Utoaji wa rambirambi na maombolezo (huzuni) inapaswa kuendelea kwa muda wa siku 3, baada ya siku hizo, maisha yanatakiwa kurejea / kurudi katika hali ya kawaida. Mtu haruhusiwi kuleta / kuhusisha hali (imani) za kishirikina (imani ya uchawi au itikadi za kidhana).

MAOMBOLEZI (EDA)

Kipindi cha Eda (maombolezi) kwa mjane (Mwanamke) wa marehemu ni miezi minne (4) na siku kumi (10). Kwa mujibu wa Kurani Tukufu, kipindi hiki kimeagizwa (kimeamuriwa) ili kumuimarisha mjane kiakili na kihisia. Wanawake wanakuwa katika kiwango kikubwa sana cha mfadhaiko katika hali kama hii zaidi kuliko wanaume na kuhitaji ulinzi dhidi ya watu ambao wanaweza kuwadhuru / kuwatumia visivyo (katika hali hii) endapo watakosa ulinzi. Katika kipindi hiki mjane hapaswi kuondoka nyumbani isipokuwa kwa sababu zisizoepukika. Kama mwanamke pekee ndiye anayeingizia kipato familia na analazimika kutekeleza wajibu wa kazi yake, anaruhusiwa kwenda nje (kazini) kutekeleza majukumu yake muhimu ya kitaaluma. Anapaswa kuvaa kikawaida na ajiepushe na kujipamba, (kujipulizia manukato yenye harufu kali) na kushiriki katika shughuli za sherehe. Anapaswa kuwa na subira (uvumilivu na ustahimilivu), kumshukuru Muumba wake na kutumia muda huu kumkumbuka Allah.

MASWALA YA KISHERIA

Kwa mtu aliyejiunga na Islam, ndugu zake wanaweza kuwa Wakristo, Mayahudi, Wahindu au imani nyingine iwayo. Baada ya kufa, mwili wa marehemu unakuwa ni mali ya ndugu zake kisheria. Waislam wanaohitaji kushughulikia mazishi yake wanapaswa kushauriana na ndugu wa kisheria wa marehemu. Ni vizuri kuandaa wasia juu ya haki ya mazishi na kutoa nakala moja kwa ndugu na nakala nyingine kwa Jumuiyya ya Waislam wa Ahmadiyya. Fedha za kutosha zinapaswa kutengwa kwa ajili ya shughuli za mazishi. Ndugu (jamaa) wanapaswa kuelezwa bayana ya kwamba ardhi (shamba) inapaswa kugawanywa kwa mujibu wa sheria ya Kiislam ya mirathi kama ilivyoelezwa ndani ya Kurani Tukufu. Mtaalam wa sheria (Mwanasheria, Hakimu au wakili) anapaswa kuombwa ushauri wakati wa kutengeneza wasia.

Mwisho.

Hongera Ahmadiyya Sekondari

Kutoka uk. 12

Amir Jamaat Ahmadiyya Tanzania Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry (katikati) akisikiliza kwa makini maelezo ya wanafunzi waliokuwa wakifanya maoneshao ya kielimu kama sehemu ya maadhimisho ua kuwapongeza wanafunzi wa kidato cha Pili 2014 .

Upande wa wanafunzi, pamoja na kuongeza jitihada katika masomo yao na kutekeleza kikamilifu mipango yote iliyoandaliwa na ofisi ya taaluma, hawakumsahau Mola wao. Saumu za suna za Jumatatu na Aklhamis lilikuwa ni jambo la kawaida tena kwa hiyari yao bila kushurutishwa na yeyote. Siku chache kabla ya mitihani, wanafunzi hawa walikaa Itkaf kwa siku nzima (kikao maalum kwa ajili ya maombi ya kuvuta Rehema za Allah) na pia kila mmoja kwa wasaa wake aliandika barua kwa Khalifa mtukufu (a.t.b.a) ili awaombee kwa Mola wake. Hivyo tunaamini kuwa, juhudi waliyoifanya wanafunzi na walimu kutekeleza mikakati ya idara ya taaluma pamoja na maombi, ndio msingi wa matokeo bora yanayopatikana katika shule yetu.

Pamoja na kuwapongeza wanafunzi wa kidato cha pili pia pongezi zilikwenda kwa wanafunzi wa kidato cha tatu ambao walifanya vizuri katika mtihani wa Tahosa mkoa wa Dar es salaam, pia kwa wanafunzi wa kidato cha kwanza walioshika nafasi tatu za juu na mwisho wanafunzi wapya (pre form one) walioshika nafasi tatu za kwanza.

Mwisho mwl aliwashukuru walimu kwa ushirikiano walioutoa hadi kufanikisha hayo, pia aliwaomba waendeleze juhudi walizozionesha ili kuleta ufaulu zaidi kwaka 2016 . pia aliwataka wanafunzi wa kila darasa kusoma kwa bidii zaidi ili mwaka 2016 kila mwanafunzi aweze kupata zawadi kwa kupata ufaulu mzuri katika masomo yake.

Nae katibu wa elimu wa Jamaat Mwl Badru Musoke akielezea juu ya umuhimu wa elimu alisema, fundisho la kwanza aliloshushiwa Mtume Muhammad s.a.w ni Iqra yaani soma. Na pia yapo maandiko katika biblia yanasema Mkamateni elimu msimuache aende zake. Kwa miongozo hiyo, hakuna bahati mbaya inayoweza kutolewa, bali kusoma ni lazima iwe kwa muislam au mkiristo.

Mwenyekiti wa kamati ya shule Mwl Abdulrahman M. Ame alipopata nafasi baada ya salamu alitoa shukurani kwa walimu kwa kuwanao pamoja katika kuliongoza gurudumu hili. Tukiwa ni wamiliki wa shule, tunayo malengo ya kuanzisha shule hii. Wapo wanaoanzisha kwa ajili ya biashara, wengine ili watajwe n.k. lakini sisi tulianzisha shule hii ili vijana wa kiahmadiyya na watanzania wote kwa ujumla wapate elimu na maadili bora. Kwa miaka mingi tumekuwa tukifikiria tutafanyaje juu ya mambo haya mawili. Pamoja na serikali kujitahidi wanafunzi wapate elimu, lakini maadili imekuwa ni changamoto kubwa. Ukiangalia wanafunzi wa vyuo, hali zao ni mbaya kimavazi n.k. hivyo tunakuombeni walimu, pamoja na kufundisha , mtusaidie juu ya maadili ya vijana hawa. Kwetu, elimu si kitu kama hakuna maadili.

Wanafunzi pia ni lazima mlizingatie hili la kupata elimu na kujitahidi kuwa na maadili mazuri. Mfano wa mfumo wa maisha, ni sawa na hali ya mtoto mchanga. Huwezi kuanza kumnyonyesha akishapita miaka mitano. Maziwa hayatakuwa faida yoyote kwake na haitawezekana. Hali kadhalika nanyi ,muda huu wa miaka mine kwenu ni muda muhimu sana kimalezi na kielimu. Mkiutumia vibaya muda huu hamtaupata tena. Hivyo zingatieni mno muda huu .msiupoteze kwa namna yoyote.

Akifunga sherehe hiyo, mgeni rasmi Amir wa jumuiyya ya waislam waAhmadiyya Tanzania na ambae ndiye mmiliki wa shule Sheikh Tahir Mahmood Choudhry alisema, Alhamdulillah, tumefikia mafanikio. Mafanikio makubwa ambayo toka mwaka jana kuwa na alama A-25 hadi kupata alama za A-40. Kwa kweli ni jambo la kumshukuru sana Allah. Kwani shule yetu imeendelea kupata maendeleo mwaka hadi mwaka. Tunamshukuru sana Allah kwa kuifanya njozi yetu kuwa kweli. Napenda kuishukuru kamati ya shule na pia walimu kwa kujitolea kwao katika kuiendeleza shule yetu. Mwaka tunaanza shule hii tulikuwa na walimu wawili tu wa kudumu, lakini leo tunao walimu wengi wa kudumu. Ni wajibu wa wazazi sasa kutekeleza wajibu wao, kwani shule haiwezi kwenda kwa juhudi ya mtu mmoja tu bali wote.

Akiwakumbusha wanafunzi juu ya wajibu wao alisema, napenda niwakumbushe muwe makini na masomo yenu kwa kipindi chote mnachokuwepo hapa. Mjitahidi katika masomo yenu bila kusahau elimu ya dini, na hata wale ambao si waislam wanao wajibu wa kuijua dini yao.

Nawapongezeni sana kwa matokeo mazuri, walimu pia Mwenyezi Mungu awabarikini sana sana kwa juhudi mliyoichukua hadi kufikia mafanikio haya.

Katika sherehe hiyo, zawadi zilitolewa kwa wanafunzi waliofanya vizuri kuanzia pre form one, kidato cha pili ambao ndio walengwa wa sherehe hizo na wale wailofanya vizuri kidato cha tatu katika mtihani wa Tahosa. Tunamshukuru sana Allah kwa matokeo mazuri waliyoyapata vijana wetu.

Wakati tukiwa bado na furaha za kusherehekea matokeo mazuri ya wanafunzi wa kidato cha pili, habari njema ya matokeo ya kidato cha nne ikatufikia. Alhamdulillahi!, Japokuwa hawajafaulu kwa asilimia mia moja lakini matokeo ni mazuri. Haya ni matokeo ya kwanza ya kidato cha nne katika shule yetu.Hoi hoi, nderemo na vifijo vya furaha vikatugubika tena kwa mara ya pili.Alhamdulillah Rabbil ‘aalamin. Kati ya wanafunzi 31 waliofanya mtihani, saba wamefeli na 24 wamefaulu kwa kupata madaraja tofauti tofauti kuanzia daraja la kwanza, la pili, la tatu na la nne. Haya ni mafanikio makubwa sana kwetu. Tunachukua fursa hii kuwapongeza sana walimu, wanafunzi na woote ambao kwa namna moja ama nyingine walishiriki katika kuhakikisha vijana wetu wanafanya vizuri. Mwenyezi Mungu awabariki sana na kuwalipa malipo mema.

Kwa upande wa wanafunzi ambao bila shaka wataendelea na masomo kidato cha tano na sita, tunawatakia kheri na tunawaomba wajitahidi ili waende mbele zaidi.

Kwa wale ambao hawakupata kuendelea waelewe kwamba hapo sio mwisho bali ndio mwanzo wa safari, wasikate tamaa bali wajitahidi kujiendeleza kwani mlango wa fadhili za Allah hauwezi kufungwa kamwe.

SHURA YA KITAIFA 2015

Amir Sahib - Jamaat Ahmadiyya Tanzania, anapenda kuwakumbusha Masheikh wa Mikoa, Marais wa Mikoa, marais wa matawi, walimu wa Jamaat nchini na Wanajumuiya wote kwa ujumla kwamba sawa na Kalenda ya matukio ya Jumuiya ya mwaka 2014/15, Majlis Shura ya Kitaifa itafanyika kwenye eneo la Jumuiya Kitonga - Dar es Salaam, siku za Jumamosi na Jumapili tarehe 25 - 26 April 2014.

Matawi yote yanatakiwa yafanye vikao vya kupendekeza ajenda za Shura pamoja na kuchagua wajumbe wa kuyawakilisha matawi yao kwenye Shura hiyo ya Kitaifa. Tawi lililo na wachangiaji zaidi ya 50, linaruhusiwa kuchagua mjumbe wa ziada kwa kila wachangiaji 50 wanaoongezeka.

Marais wote wa mikoa wanatakiwa washiriki.

Pamoja na mjumbe wa Shura atakayechaguliwa kutoka kila tawi, rais wa tawi naye pia anatakiwa ashiriki kwenye Shura ya mwaka huu.

Wajumbe wote wanatakiwa wawe wamefika kwenye eneo la Jumuiya Kitonga Dar es Salaam jioni ya siku ya Ijumaa tarehe 24 April 2014.

Ni muhimu kila tawi la Jumuiya lisipoteze nafasi yake ya kuleta mjumbe pamoja na ajenda kama watakuwa nayo.

The First Muslim Newspaper in Kiswahili Language since 1936

MapenziyaMungu

Rab. 2 - Jumd.2 1436 AH | Feb./March 2015 | Tab./Aman. 1394 HS

Kutoka Hadithi za Mtume Mtukufu s.a.w

Imesimuliwa na Hadhrat Abu Huraira r.a. ya kwamba Mjumbe wa Allah s.a.w. alisema: Ni juu yako kusikia na kutii katika dhiki yako na faraja yako, na katika furaha yako na karaha yako, na hata kama mwingine amependelewa dhidi yako. (*Muslim*).

Uchamungu ndio msingi wa maendeleo yote - Khalifa mtukufu

Na Mwandishi wetu
Dar es Salaam

Enyi mlioamini! Mcheni Mwenyezi Mungu, na mtu aangalie aliyoyatanguliza kwa ajili ya kesho, na mcheni Mwenyezi Mungu; hakika Mwenyezi Mungu Anazo habari za mnayoyatenda.

Wala msiwe kama wale waliomsahau Mwenyezi Mungu, kwa hiyo Akawasahaulisha nafsi zao. Hao ndio wavunjao sheria. (59:19-20)

Kwa kawaida mzizi wa maovu yote na ubaya wote unatokana na kutokufanya juhudi ya kuundoa kwa kudhania kwamba si jambo linalohitajika kufanya hivyo, ingawaje kutokujali huku kunapelekea kwenye makosa makubwa zaidi. Mtu kidogo kidogo anasahau mambo mema na kile kiwango ambacho kinatarajiwa kwa muumini. Hofu juu ya Mungu inafifia na imani ya mtu juu ya akhera inakufa. Kwa matendo mtu anakuwa mbali na matakwa ya kiimani.

Aya ya jirani iliyotajwa juu inatukumbusha juu ya somo hili. Mtu anakumbushwa asijali tu faida za kidunia, raha zake na mambo mengine ya kidunia tu moja kwa moja. Jambo kubwa ambalo mtu anatakiwa alijali kila wakati ni maisha yake ya baadae, kiwango chake cha imani na kushika utawa. Kuhesabiwa kwenye maisha yajayo kunatakiwa kuwe ni kiini cha kujali kwa mtu na hili pia ndilo linalopelekea kwenye maendeleo ya kimaadili. Mtu anapata maendeleo ya kiroho wakati anapokuwa makini juu ya kila anachokichuma kwa ajili ya kesho. (Akhera)

Akifafanua aya hiyo ya 19:59, Masihi Aliyeahidiwa a.s. amesema: Enyi mlioamini muogopeni Mwenyezi Mungu na kila mmoja wenu awe makini kuangalia ni nini anakitanguliza kwa ajili ya maisha yajayo. Na muogopeni Mwenyezi Mungu ambaye anazo habari za yote na anaelewa kila kitu na jiangalieni matendo yenu. Hii ina maana kwamba Mwenyezi Mungu anajua kila kitu na anatenganisha kila wema na ubaya na kamwe hakubali matendo yaliyo na mapungufu. (Tafseer by the Promised Messiah, Vol. IV, p. 338)

Hili ni lazima lieleweke na lizingatiwe. Mtu ajali zaidi kushika utawa/uchamungu na kuyaangalia matendo yake kwa umakini mkubwa pamoja na kutanguliza yale mambo ambayo yataifanya kesho yake iwe njema na sio tu kujali masuala ya kidunia kama wafanyavyo wasioamini.

Hadhrat Khalifatul Masih I r.a. aliwahi kusema Mwenyezi Mungu ametupatia msingi wa falsafa

Endelea uk. 10

Hongera Ahmadiyya Sekondari kwa matokeo mazuri kidato cha IV na II

Na Mwandishi wetu
Dar es Salaam

Tarehe 08/02/2015 shule ya sekondari Ahmadiyya ilifanya sherehe ya kuwapongeza wanafunzi wa kidato cha pili kwa matokeo bora waliyoyapata. Huu ni utaratibu uliowekwa na uongozi wa shule katika kuwatia moyo na hamasa waalimu na wanafunzi ili waendelee kufanya vizuri .

Baada ya usomaji wa Quran Tukufu iliyosomwa na Rauf M. Mua na kufuatiwa na shairi lililoghaniwa na Bilal Amir Kaluta, Makamu mkuu wa shule Mwl Hamidii Juma Kaigwa alitoa utambulisho juu ya idadi ya wanafunzi na walimu waliopo katika shule hiyo.

Baada ya utambulisho, uwanja mpana uliachwa kwa mwallimu wa taaluma Mwl Mohamed Ngunde kuelezea matokeo ya kidato cha pili 2014. Akieleza kwa muhtasari historia ya sherehe kama hii Mwl Ngunde alisema, hii ni mara ya tatu kuwapongeza wanafunzi na walimu kwa matokeo mazuri ya kidato cha pili tangu mwaka 2013. Kwa fadhila za Allah, ongezeko la ufaulu limeendelea kuongezeka mwaka hadi mwaka.

Amir Jamaat Ahmadiyya Tanzania Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry akimpatia zawadi mwanafunzi bora wa kidato cha Pili 2014 (Fadhluilahi A. Mohammed) wakati wa maadhimisho ya kuwapongeza wanafunzi hao.

Mwaka 2012 jumla ya wanafunzi 30 walifanya mtihani wa taifa wa kidato cha pili. Wanafunzi 27 walifaulu sawa na asilimia 90 na watatu (3) walifeli sawa na asilimia 10 . Jumla ya alama za juu kwa somo mwaka huo, zilipatikana “A” tatu kati ya masomo 12 yanayofundishwa shuleni hapa.

Mwaka 2013 kwa mara nyingine jumla ya wanafunzi 30 walifanya mtihani wa taifa wa kidato cha pili. Wanafunzi 29 walifaulu sawa na asilimia 96.6, na mmoja alifeli sawa na asilimia 3.4. lakini kwa Baraka za Allah, Baraza la mitihani la taifa lilimruhusu Mwanafunzi huyu aendelee na masomo ya kidato cha tatu. Jumla ya alama za juu kwa somo mwaka huo , zilipatikana “A” 25. Kukiwa na ongezeko la “A” 22.

Mwaka 2014 idadi ya wanafunzi waliofanya mtihani wa taifa wa kidato cha pili ni 28. Kwa fadhila za Allah wote wamefaulu ikiwa ni sawa na asilimia mia moja. Idadi ya alama za juu zilizopatikana ni A- 40. Kukiwa na ongezeko la “A” 15. Jumla ya wanafunzi waliopata alama hizo ni 14

Akiongelea juu ya mafanikio hayo Mwl Ngunde alisema, ongezeko la ufaulu linalopatikana kila mwaka katika shule yetu halikuja kwa bahati nasibu bali, Juhudi, mikakati pamoja na maombi kwa Allah ndio nyenzo zilizo tufikisha hapa leo. Idara ya taaluma kwa nafasi yake iliweka mikakati kadhaa kwa ajili ya maendeleo ya wanafunzi. Mitihani ya kila wiki, mitihani ya ujirani mwema katika shule za jirani, masomo ya ziada baada ya muda wa kawaida (haya walimu hujitolea kufundisha hata usiku), majadiliano ya makundi (group discussion) na pia tuliweka motisha ya zawadi kwa kila mwanafunzi atakaepata alama ya A katika somo na pia zawadi itakwenda kwa mwalimu wa somo husika. Hivyo mambo yote hayo yalifanywa kwa ushirikiano mkubwa baina ya walimu na wanafunzi, na hatimaye tumefika hapa tulipo.

Endelea uk. 11